


# Haki na itelemke

**MASOMO YA BIBLIA YA WANAWAKE MAKAO MAKUU YA KIMATAIFA**



# UTANGULIZI

Wapendwa akina dada katika Kristo

Ninafurahi sana kuwa na uwezo wa kuwasilisha kwenu toleo la pili katika tano ya Mfululizo wa Masomo ya Biblia ya Wanawake ya Kimataifa kwamba ninatarajia kuwatia moyo, kuhimiza na kushawishi kuwa wanawake wa matendo. Ninaamini sana Mungu anawaita wanawake wa imani kuinuka kwa ujasiri, kushughulikia hali halisi ya changamoto na mambo yanayowakabili wanawake na wasichana sasa hivi kila mahali ulimwenguni kote. Lazima tufanye zaidi ya kuzungumzia swala hilo! Lazima tutoe sauti kwa ujasiri, kuelewa athari zao mbaya, na kisha kujihusisha kama mshiriki katika mapambano ya kuzimaliza.

Katika wito wa Kiongozi wa Jeshi La Wokovu la Kimataifa General Brian Peddle, akinawokovu wanahimizwa "Kuchukua Jukumu" ambalo linajumuisha 'Wito kwa Huruma ya Gharama Kubwa'. Jenerali aliandika na kusema:

"Lazima tuwatetee wengine, tutafute haki, tuonyeshe ukarimu na kushiriki katika matendo ya ukombozi"

Ni katika kukabiliana na changamoto hizi kwamba mfululizo huu wa Kujifunza Biblia, " Haki na Itelemke" (Amosi 5:24) imetengenezwa. Hii ni rasilimali kubwa kwa Wanawake na wasichana wa rika zote ili kupata kuelewa kwa kina kile Biblia inachotangaza kuhusu haki ya kijamii, hali halisi isiyo ya haki ya ulimwengu wetu uliyoanguka na mwaliko wa Yesu kwetu kujiunga naye kama mwanafunzi wa haki.

“Haki na Itelemke” ('Let Justice Roll') ni mkusanyiko wa Masomo 24 ya Biblia iliyotengenezwa na wanawake 24 kutoka sehemu mbalimbali za Jeshi la Wokovu duniani. Wanawake hawa wana hamu juu ya haki ya kijamii, na maandishi yao yatakutia moyo na kukuchochea kuona ulimwengu kupitia macho ya Yesu, kuhisi shauku yake na umuhimu wa haki na kisha kuiga kwa ujasiri matendo yake katika kushughulikia dhuluma zinazotuzunguka leo.

Dunia imejaa uhasama, ubaguzi wa rangi, umaskini uliokithiri, migogoro za kidini, kutokuwepo kwa usawa wa kiuchumi, unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji wa kinyumbani, na utupu wa kiroho. Ni wakati wa kuzingatia kwa kina hukumu kibiblia ili kuangazia huruma wa Kristo, matendo na kusadiki tunapoishi kwa elimu za Kristo katika ulimwengu wa utandawazi na kuhusiana, lakini mara nyingi ulimwengu uiobinafsishwa. Ni wakati wa sisi kuungana na kuwa sauti kwa wale ambao sauti zao zimenyamazishwa na udhalimu.

Tutafanya kazi nzuri kwa watu walio katika mazingira magumu zaidi duniani tunapokabiliana na mifumo isiyo ya haki ambayo inawaweka katika umaskini na utumwa. Yesu daima anatuita kuwa wanafunzi wake, kuwa watetezi na kupigania haki katika ulimwengu wetu. Tunaitikiaje wito wake?

Masomo haya hayakusudiwi kuwa tu kwa vyama vya wanawake. Zimeundwa kutumika katika makundi ya umri wote, tamaduni, taifa, lugha na jinsia zote. Unaweza kuamua kutumia Masomo haya kwa ibada yako ya maombi ya binafsi, hata hivyo unawezachagua jinsi ya kuzitumia, tunaomba kwamba Mungu abariki na kutumia zana hii kwa njia kubwa zaidi kuliko tunavyoweza kuota au kufikiria.

Maombi yangu ya dharura ni kwamba 'tutaamka' kwa mwito wa Mungu juu ya maisha yetu ili twende zaidi ya kuona tu dhuluma, bali kupigana na kuishinda! Mungu atusaidie sote, na atupe nguvu ya kutumia Masomo haya ya Biblia kwa ajili ya heshima na utukufu wa Mungu.

Rosalie Peddle

**Kamishna Rosalie Peddle**
Rais wa Kimataifa wa vyama vya Wanawake

# WACHUNGAJI WA KWELI WA KUNDI LA MUNGU

EZEKIELI 34:1-16

ANNE MAKUMI

**'Mwanadamu, toa unabii juu ya wachungaji wa Israeli, toa unabii, uwaambie, naam, hao wachungaji, Bwana MUNGU asema hivi; Ole wao wachungaji wa Israeli, wanaojilisha wenyewe; je! Haiwapasi wachungaji kuwalisha kondoo?' (Ezekieli 34:2).**

Mchungaji ni mtu ambaye hutunza na kufuga kondoo, lakini tuangalie ni nani tunayefikiria kuwa mchungaji katika nchi yetu, kanisa letu, familia yetu au katika jamii zetu?

Huyu Mchungaji ni mtu anayetetea, kuongoza na kuwalinda watu chini yake kwa makini kama vile angewatunza kundi la kondoo. Katika jamii, wachungaji ni wale walio katika mamlaka au uongozi; watawala, viongozi kutoka ngazi za juu hadi ngazi za chini kabisa.

Wachungaji huongoza 'kundi'; wananchi au raia wao, kusanyiko la watu kanisani, wanajamii wao na familia. Wao daima wana maslahi bora ya kundi lao moyoni.


Mchungaji anatarajiwa kuongoza na kutawala kwa haki ili kundi kustawi, kama inavyosemwa katika Ezekieli 34:16, 'Nitawalisha hukumu.'

Katika Ezekieli 34:10, Bwana asema wachungaji wa Israeli ni maadui zake, kwani walijilisha wenyewe na wala hawakuwalisha kondoo waliokabidhiwa na Bwana. Zaidi ya hayo, watawala walikuwa na ubinafsi na tamaa, kujivika sufu ya wanyama wazuri na kujilisha wenyewe kwa maziwa na nyama kutoka kondoo bora, lakini bado hawakutunza kondoo. Mstari wa nne (v4) unaangazia dhuluma dhidi ya kondoo kutoka kwa wachungaji wao: ' ***Wagonjwa hamkuwatia nguvu, wala hamkuwaponya wenye maradhi, wala hamkuwafunga waliovunjika, wala hamkuwarudisha waliofukuzwa, wala hamkuwatafuta waliopotea; bali kwa nguvu na kwa ukali mmewatawala.'***

**'UPEO KAMILI WA TATIZO UNAKWENDA BILA KUTAMBULIKA KUTOKANA NA ASILI YAKE YA KUFICHWA KATIKA KUONA WAZI.'**

Kwa hiyo, tunaona kwamba Mchungaji wa kupuuza kondoo husababisha kutostawi kwa kundi. Badala yake, kondoo hutangatanga juu ya milima na vilima vya juu bila mtu wa kuwatafuta wakati wametawanyika kote nao huwa katika hatari ya wanyama wa mwitu ambao huwala - bila shaka hii ni hatari kubwa kwa kundi! Wachungaji hao pia wanaonekana kushindwa kufuata Sheria za Musa kwa kukosa kuwasaidia maskini na kujishughulikia tu kibinafsi (Kumbukumbu la Torati 15: 7-11).

Udhalimu wa kijamii kama vile utumwa na ulanguzi wa binadamu ni dhahiri katika ulimwengu wetu leo na kuathiri wengi. Ingawa upeo kamili wa tatizo huenda hautambuliki kutokana na asili yake ya kutoonekana wazi. Utumwa wa wanawake duniani kote, kunaswa kwa ajili ya ngono na kazi ya kulazimishwa, ni baadhi ya kundi ambao wamepotoshwa na wachungaji wasio wa haki. Pia tunaona dhuluma hii katika ongezeko la wanawake wanaoshambuliwa kingono au kunyanyaswa. Katika utamaduni maarufu wa hivi karibuni, tumeshuhudia harakati ya 'Mimi Pia'. Harakati hii ilifichua, na inaendelea kufichua, unyanyasaji wa kijinsia uliofanywa na wanaume wenye nguvu. Huko Hollywood, wataalamu wengi wa kike katika tasnia ya filamu walileta madai dhidi ya mtu kwa jina Harvey Weinstein. Matumizi mabaya ya mamlaka na vyeo inayoonekana katika harakati za 'Mimi Pia' ni mfano mwingine wa vitendo vya wachungaji wa kisasa wasio wa haki.



**KUJADILI:**

- Ni katika maeneo gani ya maisha yako umekabidhiwa kama mchungaji wa kundi la Mungu?
- Je, kundi lako linashamiri katika kila eneo la maisha yao chini ya mamlaka na mwongozo wako?
- Tambua dhuluma za kijamii zilizopo katika maisha ya kundi lako ambalo ungependa kusahihisha.

## MCHUNGAJI WA KWELI

Mchungaji wa Kweli ni Mungu na wachungaji wengine wote wako chini ya mamlaka yake. Ingawa awali aliwakabidhi wachungaji wa Israeli kuwatunza watu wake, anase sasa atawachunga watu wake mwenyewe, kwa sababu wachungaji wa Israeli walimwangusha.

Tunaona hapa kwamba ukandamizaji na udhalimu kwa kundi la Mungu huleta mfarakano ndani ya jamii. Wakati Bwana anachukua jukumu la kuchunga kundi lake, anaahidi kurejesha kundi lake kutoka mahali ambapo wametawanyika na kuwaongoza kwenye nchi ya ahadi.

Na Mwenyezi Mungu anasahihisha na kuondoa dhuluma zote zilizowekwa kwa watu wake. (nao wanono na wenye nguvu nitawaharibu; nitawalisha hukumu. v 16). Mungu anachunga kwa haki na yeye ni mfano kamili. Kama kundi lake, na kama wachungaji wa hapa duniani wa kundi lake, ni lazima tuhakikishe kwamba haki inatelemka kupitia kwetu. Tunaweza kuwa vyombo vya mabadiliko ambavyo hukumu itatelemkia. Kwa mfano, tunaweza kutoa mshahara wa haki au kuwa walinzi wa jamii zetu kupitia kazi za uinjilisiti. Tunaweza kuwaambia wengine kuhusu dhuluma za kijamii, kunena kwa niaba ya wale ambao hawawezi kusema wenyewe. Tunaweza kutumia ufahamu wetu kuwaelimisha wengine na kutumia njia salama za kuripoti.

Bwana, nifanye chombo chako ambacho hukumu inaweza kutiririka Kwa kundi ulilonikabidhi.

## ANNE MUKAMI

TERITORI YA KENYA MASHARIKI



Anne ni Meneja wa Mradi wa Kupambana na Ulanguzi wa Binadamu katika Jeshi la Wokovu Kenya Mashariki. Pia alikuwa mwanachama wa Kikosi Jeshi la Kimataifa la Kupambana na Ulanguzi wa Binadamu kilichoanzishwa ili kuhimiza na kutumia rasilimali ili kuleta majibu makubwa zaidi ili kupambana na biashara haramu ya binadamu. Anne ana shahada ya uzamili katika Sayansi kutoka Chuo Kikuu cha Witwatersrand, Johannesburg, na ana uzoefu mkubwa wa kufanya kazi kwa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali katika maeneo yenye maslahi ya binadamu na utafiti wa afya.

# UPENDO KATIKA MATENDO

WARUMI 12:9-21

MEJA ANUGRAH M. MASIH

**‘Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema’ (Warumi 12:21).**

Haki inawezaje kutelemka wakati watu wamejaa chuki; wakati wanawake na wasichana wanaponyanyaswa kingono, kushambuliwa, kubakwa na kuuawa; wakati watu wana njaa, wakati kuna usambazaji wa rasilimali za kiuchumi usio sawa na nguvu za kisiasa; wakati mataifa yanajihami kwa nguvu za nyuklia na silaha?

Warumi: 12: 9-21 inatoa matendo ya kuishi maisha sahihi na ya haki: 'Shinda uovu kwa wema'(v21). Lakini hii inawezekana tu ikiwa matendo yetu yote yanachochewa na upendo. 1 Petro 4:8 inatuhakikishia, 'Juu ya yote, pendaneni kila mmoja kwa undani, kwa sababu upendo hufunika juu ya wingi wa dhambi'. Paulo aliandika barua yake kwa Warumi miaka 58 baada ya Yesu akiwa Korintho. Paulo alikuwa bado hajatembelea Warumi wakati aliandika waraka huu, lakini alikuwa na hamu kubwa ya kuwatembelea Warumi (Warumi 1:11). Alienda katika mji huo miaka mitatu baada ya kuandika barua hii. Paulo alijua kuhusu mgogoro kati ya Wakristo wa KIyahudi na Mataifa katika Kanisa la Warumi. Wakristo wa Kiyahudi waliamini kwamba, ili kuwa Wakristo, watu wa mataifa walipaswa kuwa Wayahudi kwanza kwa kutekeleza desturi na mila zote za Sheria ya Musa, hasa mazoea ya kidini. Tukitumia mistari hii kwa muktadha wa kisasa, tunaweza kuwa na ulimwengu ambapo hukumu ya haki itatelemka inapatikana.

Hebu tuchunguze Warumi 12:9-21 chini ya mada 'upendo katika matendo':


**1. Upendo wa dhati: Warumi 12:9-12**

Upendo ni sifa muhimu za Mungu wetu wa Utatu, ambao ametupa sisi pia. Upendo ni muhimu (1 Wakorintho 13: 1-13), upendo ni mkuu wa fadhila zote na ni mojawapo ya matunda ya Roho (Wagalatia 5:22). Katika aya hii Paulo anawahimiza Wakristo kufuata upendo wa dhati, kuchukia uovu na kutenda mema katika uhusiano wao na waumini wengine. Kupitia matendo ya upendo tunaweza kuwa na mahusiano sahihi na ya haki na wengine, na Mungu na dunia nzima. Katika Amri kuu (Mathayo 22:36-40) Yesu anatufundisha kwamba, ili kumpenda Bwana Mungu wetu kwa moyo wetu wote na kwa roho zetu zote na kwa akili zetu zote, lazima pia tupende jirani zetu kama sisi wenyewe kwa sababu wanadamu tumeumbwa kwa mfano wa Mungu. Jirani ni mtu ambaye anahitaji na anatafuta msaada wetu. Tunapoishi katika jamii zetu, makanisa, nchi za dini nyingi na muktadha wa tamaduni mbalimbali, hebu tuone sura ya Mungu katika wale wanaoteseka. Hebu tuthamini na kuheshimu kila mmoja kwa mwingine kama tunavyotarajia kupendwa na kuheshimiwa na wengine.

**2. Upendo wetu kwa jamii yetu: Warumi 12:13-18**

Wafilipi 2:5 inatusaidia kuzingatia kuwapenda watu katika jamii yetu kwa matendo yetu mema: 'Katika Mahusiano yako na wengine, kuwa na mawazo sawa na ya Kristo Yesu.' Tunaweza kushangaa kuhusu mawazo ya Yesu, na tutaipata katika mistari iliyotangulia.

## 'HEBU TUTHAMINI NA KUHESHIMIANA TUNAVYOTARAJIA KUPENDWA NA KUHESHIMIWA NA WENGINE.’



**KUJADILI:**

- Hebu tuchunguze maisha yetu. Je, kwa kweli tunamwiga Kristo Yesu? Je, tuna mawazo sawa na mawazo Yesu alikuwa nayo?
- Inaweza kuwa vigumu kuwasamehe maadui zetu na kuwapenda watesaji wetu. Tunaweza kupata wapi nguvu na roho ya msamaha na upendo?
- Inamaanisha nini, katika maisha yetu binafsi, kuwa na upendo wakujitolea wa Yesu?

Kuwa mfuasi wa Yesu Kristo, Paulo anahimiza kanisa la Warumi kuwa na sifa au mawazo ya Yesu. Leo anatuhimiza sisi pia, kujiweka sawa na sifa hizi za kuleta Ufalme wa Mungu ambao ni wa haki na kweli. Sifa hizi ni pamoja na:

1. Kushiriki na wengine
2. Kufanya mazoezi ya ukarimu
3. Kuwabariki watesi wako
4. Kuepuka kulaani
5. Kufurahi pamoja na wale wanaofurahi
6. Kuomboleza na wale wanaoomboleza
7. Kuishi kwa uwiano na kila mmoja
8. Kuepuka kiburi
9. Kushirikiana na watu wa chini
10. Kutokuwa na majivuno
11. Kufanya kile unachotaka wengine wakufanyie.

Hebu tumuige Kristo Yesu. Katika ilani ya Nazareti (Luka 4:18-20) Yesu alisema kusudi lake kuja duniani. Aliishi kulingana na tamko hili miaka yake mitatu na nusu ya huduma duniani. Yeye Alitangaza habari njema kwa maskini, akawaponya vipofu, viwete, na wa ukoma, alitoa pepo, alifufua wafu, wakafariji waliao, alibariki wale waliomtesa. Akawa sauti, mtetezi na mlinzi wa walioonewa, waliofinyiliwa chini na maskini. Alivuka mipaka ya jinsia na kuwasamehe wale waliomtukana na kumtesa.

**3. Upendo wetu kwa wale wanaotutesa: Warumi 12:19-21**

Tulipokuwa wenye dhambi hatukuwa na njia ya kuondoa dhambi na kurejesha uhusiano wetu uliovunjika na Mungu. Kwa sababu ya upendo wake na huruma ya neema, Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee. Mwana huyo alichukua makosa yetu yote mwenyewe. Wafilipi 2: 1-11 inatuambia kwamba Yesu alijiondoa mwenyewe. Neno la Kigiriki kenosis linamaanisha alijitoa mwenyewe, na hiki ndicho Yesu Kristo alifanya. Kwa sababu ya makosa yetu aliteswa. Watu walimdhihaki, wakamtemea mate, wakavua nguo zake na kupiga kura kwenye mavazi yake. Lakini hakutafuta kulipiza kisasi kwa wale waliomtesa wakati wa kesi yake, njiani kuelekea Kalvari na msalabani. Badala yake aliomba kwa Baba yake wa mbinguni, akisema: 'Baba awasamehe kwa sababu hawajui wanachokifanya.' Ingawa alikuwa mwanadamu kamili na Mungu kamili, alijiona kuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu na alibaki mwaminifu hadi kufikia hatua ya kifo na kutoa wokovu pia.



Mungu wa upendo, tunakuomba uondoe matendo yote mabaya kutoka kwa maisha yetu na tunaomba kwamba tuweze kuonyesha tabia zako zote na mfano wako. Amina.

**MEJA ANUGRAH M. MASIH**
TERITORI YA INDIA KASKAZINI
Meja Masih ni Mkina Wokovu wa kizazi cha nne na afisa, anayehudumu kama Katibu wa Rais wa Vyama vya Wanawake, anayeishi 'New Delhi'. Anasema: 'Mama yangu Aliniweka wakfu kwa ajili ya huduma ya Mungu nilipokuwa tumboni mwake na baadaye katika ujana wangu Mungu aliita mimi binafsi kuwa mtumishi wake. Napenda kusoma vitabu na kuimba. Mwaka wa 2019 nilimaliza Shahada yangu ya Uungu. Mungu amenibariki mimi na mume wangu, Meja Amrik Masih, na mabinti wawili, Angleena, 15, na Catherine, 12.'



# MIOYO YA UFALME

## MATHAYO 6:1-15 NA MATHAYO 7:1-12

LUTENI CHRISTINE TURSI

Unaweza kosa kupenda hili, lakini ukweli ni kwamba vifungu hivi havihusu udhalimu na giza ulimwenguni na wito wetu wa kufanya kitu kuhusu hilo. Vinahusu utangulizi na uingiliaji wa Mungu kwa sababu tunafanya sio tu kuishi katika ulimwengu wa fujo, bali nasi tumeharibiwa. Hata hivo, habari njema ni kwamba Mungu hasemi kuwa tumevunjika mioyo sana hata tukashindwa kumsaidia kujenga ufalme wake duniani. Badala yake, anasema, napenda nianze kwa kujenga Ufalme moyoni mwako, na mengine yatafuata (Mithali 4:23). Je, hiyo sio habari za kushangaza? Mbingu katika ulimwengu inaweza anza na wewe na mimi!

Sasa basi, tunaanzia wapi? Kwa kumruhusu Mungu kuchunguza moyo wako wote, hata kona zake za mbali ambapo tunaweka matakwa yetu na ndoto zetu, nia na matarajio yetu ya kweli. Hapa ndipo mawazo yanaweza kutawala na kunong'ona: 'Angalia yote niliyoyafanya! Je, watu wanaona juhudi zangu, haki yangu, kupigania haki kwangu, upendo wangu kwa watu wote? Ujira wangu uko wapi?

Tusipokuwa makini, minong'ono hiyo inakua kubwa na inakuwa kitu pekee tunachosikia na kukifanyia kazi. Tusipoacha Mungu atawale, mawazo yetu yatatuongoza kwenye uharibifu wa kila kitu tulicho nacho na tunachokufanya, hata kama kweli tulifanya hivyo ili kumpendeza Mungu mara ya kwanza. Mawazo yetu yataharibu motisha yetu, vipaumbele vyetu na nia zetu, itaharibu mioyo yetu na kutuongoza mbali na Mungu. Bila hata kuitambua, hatutajenga tena ufalme wa Mungu duniani lakini yetu wenyewe, na kwa aina hiyo ya ufalme wa kujihudumia hakuna thawabu ya milele (Mathayo 6:1).


Je, Yesu – Yule anayetazama mioyoni mwetu – anasema nini ili kuzuia jambo hili? Anasema: Usitoe kiasi chochote ya fedha kwa ajili ya watu kupongeza ukarimu wako (Mathayo 6:2). Badala yake, toa kila kitu ulichonacho kwa sababu wameelewa kwamba ni kwa sababu ya kila kitu nilichokupa (1 Yohana 3:16).

Wala msiombe maombi ya unafiki ili watu wawasifu (Mathayo 6:5); uliza, bisha, tafuta kwa sababu unanipenda, mnanitazamia mimi na Ufalme wangu (Mathayo 6:6). Najua moyo wako, najua unachohitaji hata kabla ya kuniuliza (Mathayo 6:8), kwa kuwa ninakupenda, nitakupa yote uombayo (Mathayo 7:11).

Usiwahukumu wengine au kuonyesha udhalimu katika maisha yao kabla ya kuangalia maisha yako na moyo wako mwenyewe (Mathayo 7: 1-4). Fanya hii kuwa desturi ya maisha yako, 'fanya kwa wengine kile ungependa wakufanyie' (Mathayo 7:12): Hutaki wakuhukumu wewe au kukupenda wewe na ajenda, hutaki watumie huzuni yako au mateso kwa madhumuni yao wenyewe, sawa? Kwa hiyo, wapende, wapende tu, kwa sababu unanipenda na kwa sababu nimekupenda kwanza (Mathayo 7:12; 1 Yohana 4:19).

Je, unyenyekevu huu unamaanisha kwamba hakuna mtu anayeweza kujua kuhusu mapambano yetu kwa ajili haki ya kijamii? La. Kwa kweli, tunahitaji kuzungumzia mapambano yetu dhidi ya dhulma ya kijamii ili kuhamasisha, kuwatia wengine motisha na kuchanga pes. Hata hivyo, kabla ya vyombo vya habari 'kuchapisha' kwenye blogu tuliyonayo imeandikwa, kabla ya kuanza mazungumzo au kupanga mradi, hebu tumwombe Mungu aangalie nia zetu, malengo na makusudi yetu kwanza. Tunatarajia kufikia nini? Je, tunataka umaarufu na idhini?

**‘Tunahitaji kuongea kuhusu vita dhidi ya udhalimu wa kijamii, ili kuhamasisha, kuwatia motisha wengine na kuchanga pesa.’**



**KUJADILI:**

- Nia na kusudi yako katika kupigania haki ya kijamii ni nini? Je, unajenga Ufalme wa Mungu? Usijali kama majibu yako si makubwa zaidi? Mungu anaweza kurekebisha hilo. Muulize afanye hivyo.
- Pamoja na wenzetu, tunawezaje kusaidiana kuzuia mawazo zetu na kwa unyenyekevu kujenga tu Ufalme wa Mungu badala yetu wenyewe? Tunawezaje kutembea pamoja, kumfuata Yesu pamoja na kuwa Wajenzi wa ufalme pamoja?
- Jifunze na uombe Sala ya Bwana. Ruhusu Roho Mtakatifu kusafisha moyo wako, kukujaza na motisha zake, nia na vipaumbele. Shiriki ndoto na maono ya mahali unapoishi na jiruhusu mwenyewe kuongozwa na Roho.

Kwa hashtegi tulizua mwelekeo? Kuwa na picha ya kitu tulichosema au kilishirikishwa kote ulimwenguni, au majina yetu kukumbukwa na vizazi vijavyo? Au tunataka tu kumpenda Mungu na watu kwa moyo mkunjufu?

Ili kuweza kufanya la kutangulia, tunahitaji kuwa watu wapya kwanza. Watu wa ufalme wenye mioyo ya ufalme. Haya yanaweza kutokea tu ikiwa tutaacha kujifikiria wenyewe na kuanza kufikiria juu ya Yesu. Hiyo ni kusema, tunapaswa kufa kwa sisi wenyewe na kuishi kwa ajili yake. Hivyo ndivyo Agano la Kale na, hata Biblia nzima kuashiria. Na ndivyo asemavyo Yesu katika vifungu hivi: Usiwe mfalme wa maisha yako mwenyewe. Badala yake, acha niwe Mfalme na Ufalme wangu utakuja, mapenzi yangu yatatimia, moyoni mwako na duniani kama ilivyo mbinguni (Mathayo 6: 9-13). Wakati ambayo yatatokea, tutaweza kuwapenda wengine kwa moyo wote na haki itatelemka kama mto, kweli kama mkondo wa mto usioshindwa (Amosi 5:24) kwa sababu ufalme wake utajengwa, lakini sio kwa nguvu zetu wenyewe. Na hiyo hakika, kwa kweli, itakuwa Mbingu duniani.




Bwana, unaona ndoto and kung'ang' ana kwangu; nifanye niwe mpya, nisaidie kuwa mtu unayeweza kutumia kupenda wengine, kupambana na udhalimu, kujenga ufalme wako duniani. Nipe moyo wa ufalme.


**LUTENI CHRISTINE TURSI**

TERITORI YA UJERUMANI, LITHUANIA NA POLAND


Christine Tursi ni luteni anayejaribu kueneza Nuru ya Mungu katika kitongoji cheusi sana cha Hannover, Ujerumani. Yeye ni Mjumbe wa Injili, mpiganaji wa haki, mkina wokovu kwa moyo, lakini zaidi ya kitu chochote yeye ni mfuasi wa Yesu.



# UPENDO TU

HOSEA 2:16-23
MEJA MARGARET DAVIS

Ninapenda hadithi nzuri ya kupendo. Habari tamu za upendo zinazowasisimua wanandoa, wakitangaza upendo wao, wakishind changamoto za ndoa na kuishi kwa furaha milele. Inachangamsha moyo wangu. Kwa sababu Mungu ni upendo, ametuwekea upendo - kuupokea na kuutoa - kuufuata - kuupigania na kuufurahia. Onyesho kamili la upendo hutoka kwa Mwenyezi Mungu; anaweka kiwango cha juu (1 Wakorintho 13: 4-8). Kwa sababu ya ubinadamu wetu, tunaonyesha upendo ambao umepungua kwa kiwango hicho, na mara nyingi husababisha maumivu ya moyo, mateso na ukandamizaji. Mifumo ya ulimwengu huu pia ipo chini ya ujenzi potovu wa upendo ambao unashindwa kufikia kiwango kitakatifu cha Mungu. Kama Mungu wa haki, tunaweza kukubaliana kwamba ni mapenzi yake kwa hili kuwekwa sawa. Katika kifungu chetu cha Maandiko, tutazingatia mada hii ya haki na msingi wake katika upendo kamili wa Mungu.

Nabii Hosea alihudumu katika miaka 30 kabla ya kuanguka wa ufalme wa kaskazini wa Israeli katika 722 (Kabla ya Kristo). Unabii wake ulielekezwa hasa kwa watu wa ufalme huu ambao walikuwa wameacha kuabudu Mwenyezi Mungu, na kuanguka katika kuabudu sanamu, kuabudu Baali, miungu ya Kanani. Hii iliuharibu moyo wa Mungu, na aliitumia hadithi ya Hosea na Gomeri kuwaeleze watu wake kwa kina usaliti wao na matokeo ya dhambi zao.


Katika mlango wa kwanza wa Hosea, Mungu anamwamuru nabii wake kumuoa Gomeri, mwanamke mwenye maazimio, na kuwa na watoto pamoja naye. Watoto hao watatu waliozaliwa wakati huo wa ndoa yao walionekana kuwa watoto wa kutokuwa waaminifu, kusisitiza kiwango cha kutoamini kwake. Walipewa majina yanayoashiria hukumu ya haki ya Mungu kama matokeo; 'Mungu Hupenda', 'asiye kupendwa' na 'wasio watu wangu'.

**'ROHO WAKE MTAKATIFU ANA TUPA NGUVU SISI KUPENDA KAMA ALIVYOPENDA; KUWAOKOA WANAOANGAMIA, WANAONYANYASWA, WASIOELEWEKA NA WALIO POTEA.'**

Kwa sababu ya upendo wa ajabu wa Mungu, hata hivyo, hadithi haikuishia hapo. Haja yake haikuwa kwa ajili ya uharibifu wa watu, lakini urejesho wao. Yeye ni Mungu, ambaye hutenda yaliyo ya haki! Katika mlango wa 3 tunaona Gomeri amemwacha Hosea na watoto wao na anaishi katika dhambi na mwanaume mwingine, licha ya maonyo yaliyoyapokea. Hata hivyo, Mungu anamwambia Hosea aende kumchukue mkewe, ambaye alimnunua kwa vipande 15 ya fedha, vichaka vitano vya shayiri na kipimo cha mvinyo, maana yeye sasa alikuwa ameanguka katika utumwa wa ngono. Na kwa hiari anarudi kwa nyumba yake ya ndoa.

Hosea 2:16-23 inatuonyesha matokeo ya ajabu ya uamuzi wa Gomeri wa kurudi kwa mumewe kwa uaminifu. 'Tena siku hiyo itakuwa,' asema BWANA, 'utaniita "Ishi" wala hutaniita tena "Baali". (Hosea 2:16)

Hili ni rejeleo la kwanza katika Maandiko kwa Mungu kama mume wa watu wake na tofauti kati ya 'mume' na 'bwana' haipaswi kukosa. Baali katika Kiebrania hutafsiriwa kama 'mume' pamoja na 'bwana'. Uhusiano kati ya Watu wa Mungu na Baali ulikuwa mmoja wa mabwana wakali kwa utumwa,



**KUJADILI:**
- Kwa kiwango cha 1 - 10 ungepima kiwango chako cha kujitolea kwa Mungu kwa wakati huu?
- Je, kuna mambo yoyote au watu ambao wanaweza kuchukuliwa kuwa sanamu katika maisha yako, kukutoa katika umaarufu na uhusiano wako na Mungu?
- Ni kwa nani unahitaji kupanua 'upendo tu' (rehema na msamaha)?

Hata hivyo, Mungu kama mume wao angewaonyesha upendo na urafiki wa kweli, kuhakikisha usalama na kuwapa mahitaji yao. Wale ambao walitumikia Baali walikuwa chini ya utamaduni wenye sumu ya uvivu (Hosea 4:14), mila ya ukeketaji wa binafsi (1 Wafalme 18:28) na hata dhabihu ya binadamu (Yeremia 19: 5) - upotovu wote wa upendo, urafiki, na utakatifu wa maisha uliotawazwa na Mungu wetu mtakatifu.

Kwa hiyo, kwa moyo wa huruma na msamaha Mungu alitoa urejesho kwa Gomeri katika tamko linalopatikana katika mstari wetu muhimu:

> “Nami nitakuposa uwe wangu milele;
> Naam nitakuposa kwa haki, na kwa hukumu,
> Na kwa ufadhili na kwa rehema” (Hosea 2:19)

Ni ahadi nzuri! Licha ya kukataliwa kwake Hosea na usaliti wake wa agano la ndoa yao, Mungu aliahidi kumkaribisha tena na kuanza kile kitakachokuwa uhusiano wa upendo ambao ungedumu milele – agano ambalo kamwe halingevunjwa.

Zaidi ya hayo, uhusiano ungekuwa na sifa ya haki, upendo na huruma. Sifa hizi ni mfano wa tabia takatifu za Mungu - hawezi kupenda kwa njia nyingine yoyote! Yote ambayo Gomer alikuwa ana uzoefu nayo katika mikono ya Baali ingesahihishwa na kufanywa haki na Yule aliyempenda kama alivyofanywa kupendwa - katika utakatifu na usafi. Mahitaji yake matakatifu ya uaminifu pia yatambuliwe katika uhusiano wao wa upendo.

Kupitia hadithi ya Hosea na Gomeri, Mungu alikuwa akiwaita watu wake kurudi na kujipeana kikamilifu kwake Mungu. Nusu ya upendo katika uhusiano huu uliolinganishwa na uzinzi wa kiroho na haukuwa mzuri wa kutosha kwa Mungu ambaye ana wivu kwa watu wake (Kutoka 20:5). Haja yake ilikuwa ni kwa ajili ya watu wake kurudi kwake kwa mioyo yao yote. (Yoeli 2:12) Kukubalika kwa upendo wake na mapenzi yake ingewaokoa kutokana na ukandamizaji wa dhambi na kuzaa haki takatifu katika maisha yao na katika dunia.

Ujumbe wake kwetu leo ni mara mbili: 'Pokea upendo wangu wa haki na ushiriki na wengine.' Roho Wake Mtakatifu anaweza kutuwezesha kupenda kama alivyopenda; kuwaokoa wanaoangamia, wanaodhulumiwa, wasioeleweka na wanaopotea, na kupanda mbegu za haki katika ulimwengu unaougua ili kuwa sawa.



Bwana, ahsante kwa upendo wako usio na masharti, wa kupendeza na wa milele. Nakuhitaji kama mpenzi wa nafsi yangu na mume wangu milele. Nisaidie kuwapenda wengine kama ulivyonipenda. Amina.

## MEJA MARGARET DAVIS

TERITORI YA MAREKANI MASHARIKI

Margaret na mumewe David kwa sasa wanahudumu kama viongozi wa Sehemu katika Idara ya Massachusetts katika Teritori ya Marekani Mashariki. Maagizo yaliyopita yamejumuisha Vikao, Viongozi wa vijana kwa Sehemu na Vyama vya wanawake, na Chuo Cha Maafisa. Anapenda muziki, historia na usafiri. Margaret na Daudi wana mabinti wawili wazima, Brittany na Alexa, ambao wote wanafanya kazi katika uwanja wa haki ya kijamii.



# KUWATETEA MASKINI

YEREMIA 22:13-18
DKT. JOY AGPAOA-ORTEGA

**''Alihukumu maneno ya maskini na mhitaji; hapo ndipo alipofanikiwa, Je? Huku siko kunijua, asema BWANA?" (mstari wa 16).**

Watu wengi katika ulimwengu wetu wanateseka kutokana na udhalimu na wanaumia na kuvunjika mioyo, hawana tumaini na wamekata tamaa. Baadhi ya watu hufanya kazi kwa bidii lakini hawapati mshahara mzuri; wametengwa na ni waathirika wa udhalimu. Baba yetu wa Mbinguni anatuambia tufanye kile kilicho cha haki na ukweli: *haki na itelemke*.

## MAANDIKO YANASEMA NINI:

Katika Yeremia 22:3, Mungu anawaagiza wafalme waovu, 'fanyeni hukumu na haki, mkamtoe yeye aliyetekwa kwa mikono ya mdhalimu; wala msiwatende wageni mabaya, wala yatima, wala mjane, wala kuwadhulumu wala msimwage damu ya mtu asiye na hatia katika mahali hapa"

**'UKAKAMAVU WETU WA NGUVU NA UPENDO WA KUFANYA HAKI INAWEZA KUFANYA UTOFAUTI MKUBWA KATIKA JAMII.'**

Kifungu chetu cha somo kinanaonyesha chuki ya Mungu kwa matendo ya udhalimu yaliofanywa na Mfalme Yehoahazi (pia anajulikana kama Mfalme Majumuisho), mwana na mrithi wa Mfalme Yosia. Mfalme kijana alipuuza mageuzi ya baba yake na kuwakandamiza maskini 'atumiaye utumishi wa mwenzake bila ujira, wala hampi mshahara wake' (mstari wa 13).

Uovu wa Mfalme Yehoahazi unawakilisha maambukizi ya udhalimu wa kijamii wakati huo. Matajiri walikanyaga juu ya haki za maskini na haki ikafichwa. Mungu katika hasira yake alitumia utumwa kuwafundisha watu wake masomo muhimu kuhusu ukamilifu na haki. Kutokana na hili tunaweza kujifunza:


1. Mungu ako kinyume na uovu, udhalimu na matendo mabaya, hasa inapofanywa na wale walio katika mamlaka.
2. Mwenyezi Mungu huwapendelea waliotengwa na kuwatetea maskini.
3. Mwenyezi Mungu anamwaadhibu mdhalimu kwa kiwango kamili, hivyo kwa kutufundisha kwamba haki inahusishwa na kufanya kile kilicho sawa na haki.

## KIOO CHA UKWELI:

Katika kukabiliana na kila tendo la ukandamizaji, kuchukuliwa visivyo ya haki, ubaguzi na udhalimu wa kijamii ni huruma na upendo wa Mungu. Maskini kamwe hawako peke yao. Mungu anasema wazi katika mstari wa 16 kwamba atatutetea na atakuwa Mungu wa haki na usawa miongoni mwa watu wake.

Azimio letu, na upendo wetu, kwa kufanya kile kilicho sahihi na haki, inaweza kuleta utofauti mkubwa katika jamii. Haki huanzisha uadilifu na inasababisha kukubalika, bila kujali asili yetu, hadhi yetu, na utu wetu.

Je, tunapaswa kuwa na mioyo migumu, kufunga masikio yetu kwa dhuluma? Je, kuna nyakati ambazo Mungu



**KUJADILI:**

- Mungu alionyeshaje haki miongoni mwa watu wake katika Agano la Kale? Linganisha hali hii na jinsi tunavyotafuta haki leo.
- Ni dhuluma gani unazoziona katika jamii yako?
- Ulijibuje uzoefu wa kibinafsi wa udhalimu?
- Je, umeona dhuluma yoyote katika Kikao chako? Ulikabilianaje na hali hiyo?
- Ni ufahamu gani mpya ambao umepokea kupitia utafiti huu wa biblia?

Tunapokabiliana na changamoto za kudhulumiwa na kutotendewa haki, je, tunatafuta kulipiza kisasi kwa wasio haki? Je, ni mkondo upi wa hatua tunaochukua? Je, tunafanya kile kilicho sahihi na cha haki? Hata wakati hakuna mtu anayetuona? Mungu anataka tufungue mioyo na akili zetu na kuwa makini na matendo yetu kwa wengine.

Tukijua kwamba Mungu ni mkuu katika maisha yetu, hebu tufanye kile kilicho sahihi na cha haki. Anataka tumiliki sifa za Yesu ambaye kamwe hakushindwa kutoa haki kwa maskini dhidi ya Mafarisayo na Masadukayo.

Baba yetu wa haki, ni maombi yangu kwamba haki iwe kipaumbele kwangu. Nifundishe kufanya kile kilicho sahihi na haki, na kuwa chombo kamili, cha jinsi haki itatelemkie katika familia yetu, kwa marafiki na kwa jamii nzima. Amina

## DKT JOY AGPAOA-ORTEGA

**UFILIPINO**

Askari wa furaha huko Kikao cha Palmera mjini Bulacan. Yeye ni binti wa maafisa wastaafu na ni daktari mwenye leseni na mtaalamu wa kisukari akifanya mazoezi ya dawa za ndani.



# KUJIFUNZA KUFANYA VIZURI

ISAYA 1:15-18

CAROLINE HMINGTHANZUALI

Nanyi mkunjuapo mikono yenu, nitaficha macho yangu nisiwaone; naam, muombapo maombi mengi, sitasikia; Mikono yako imejaa damu! Jiosheni, jitakaseni. Uondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya. Jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki. Wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane. "Haya njoni tusemezane asema BWANA, Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji, zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.' (Isaya 1:15-18).

## 'KRISTO... ANGELIMKIRI KAMA MTU AMBAYE ALIYE WA THAMANI KUBWA NA KUHESHIMIWA.'


Kifungu chetu cha somo hufanyika wakati wa utawala wa Mfalme wa Yuda, Uzia. Kukosekana kwa uchokozi kutoka kwa falme jirani za Misri na Ashuru pia kutoka ufalme wa kaskazini wa Israeli, ufalme wa Yuda uliongoza katika biashara na uchumi. Wasomi wanaokua mijini walifurahia utajiri unaoongezeka wa taifa wakati wale wa kiwango cha chini na wakaazi wa vijijini waliachwa nje kutokana na faida hiyo. Matajiri na wenye nguvu waliwatumia wanyonge kwa kuchukua mashamba yao kwa amri ya serikali. Kuongezeka kwa kodi na aina nyingine za ukandamizaji. Ni katika kurudi nyuma kwa kutokuwepo kwa usawa huu wa kufurahisha kwamba nabii Isaya aliinua sauti ya Mwenyezi Mungu.

Licha ya kupuuza taabu za raia wenzao, matajiri na wenye nguvu hata hivyo waliendelea kumheshimu Mungu wakimuomba na kumuabudu. Mwenyezi Mungu aliye tenda uadilifu, mwenye kurehemu alitambua unafiki na kuongea dhidi yake kupitia Isaya. Hakuridhika na kujitolea kwao kwake wakati kitendo chao hakikuonyesha upendo na ukarimu kwa wale walikuwa karibu nao.

Katika miaka yangu ya kufanya kazi na wanawake katika mazingira magumu, nilikutana na kesi ya mwanamke mwishoni mwa miaka yake ya thelathini ambaye aliingizwa kwenye makazi yanayoendeshwa na serikali na nilihusishwa nayo. Alikuwa mhamiaji haramu kutoka Myanmar ambaye alikuwa na mtu moja tu wa uhusiano kidamu huko Aizawl, India, binamu ambaye hangeomba msaada. Kwa kuongeza kwa taabu yake, alikuwa mzazi wa pekee wa msichana mwenye umri wa miaka minane na mtoto mchanga ambaye alilazimika kupeana alelewe na watu wengine kwa kulazimishwa na binamu yake. Jeshi la Wokovu liliitwa ili kumsaidia. Alitengana na binti yake ambaye aliingizwa kwa makao ya wasichana yaliyosimamiwa na Jeshi la Wokovu kama ilivyoamuliwa na mamlaka ya kuasili Watoto (*Authority of adoption*). Ni dhahiri kuwa uamuzi huo ulifikiwa kwa kuzingatia ulevi wa zamani wa mwanamke huyo na si juu ya hali yake ya sasa.

Kesi yake mara nyingi imenifanya nishangae kama tulishindwa kumsaidia kama Mwili wa Kristo. Je, tulishindwa kuwa sauti yake wakat alihitaji msaada? Je, tulisimama kwa ajili yake katika harakati zake za kumshikilia mtoto wake? Je, tulimhukumu kwa kosa lake la zamani na kukosa kuona azimio lake la sasa la kuwa mama mwema? Je, tulimpa fursa ya kuwa mamamwema na kumsaidia kufikia lengo hilo? Kwa kweli, sidhani kama tulifanya hivyo. Je, msaada tuliompa ni ule tulifikiria anhitaji au kile alichotaka? Pengine. Kama ni Kristo angejibu haja yake, angemtambua kama mtu ambaye thamani yake ilikuwa ya kuheshimiwa.

Labda tunahitaji kurejelea sababu za kutekeleza huduma zetu za kijamii kama Jeshi la huruma. Je, ni upendo wa Kristo ambao unatulazimisha kutekeleza huduma kama hizo au tunapeana tu jibu ya kibinadamu kwa haja tunayoiona?



**KUJADILI:**

- Ni dhuluma gani za haraka ambazo ninaziona karibu nami?
- Je, mimi ni sehemu ya dhulma hizo?
- Ninasimama wapi kuhusiana nazo?

Mungu alizungumza na watu wa Yuda kupitia kwa nabii wake akisema, 'Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya; ***17*** jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane.' (mstari wa 16-17). Vifungu hivi vinaashiria kugeuka kwa ufahamu wamapenzi, kusababisha uamuzi ambao utafuatwa na vitendo vinavyotafuta haki, kuwezesha, kuinua, kutetea nakutetea taabu ya wanyonge na wasio na sauti.

Katika mstari wa 18, Mungu mwenye huruma milele hutoa fursa ya upatanisho kwa watu ambao matendo yao yanachukiza. Kupitia nabii Isaya, alitabiri upatanisho alioutayarisha kwa ukarimu kwa ajili ya dhambi zetu kwa damu ya Mwanawe, Yesu Kristo. Ikiwa tu tutatafuta mapenzi yake na kufanya uamuzi wa fahamu kugeuka mbali na vitu vinavyomuumiza.

Tukumbushwe kwamba Mungu asiyebadilika anakumbukwa na dhulma katikati yetu leo kama vile ilikuwa katika siku za Isaya. Watu ambao mistari hii inane kwao, hata hivyo, wamebadilika. Sasa ni kwa wewe na mimi kwamba mistari hii takatifu inazungumzwa. Kama Wakristo, matendo yetu ni lazima kuchipuka kutoka kina ambacho ni zaidi kuliko ubinadamu wetu. Katika 1 Wakorintho 16:13, Paulo aliwaomba waumini huko Korintho kuwa walinzi, kusimama imara katika imani, kuwa na ujasiri na nguvu na kufanya kila kitu katika upendo. Katika pumzi hiyo hiyo, 1 Yohana 4:8 inatuambia kwamba Mungu ni upendo. Kwa hiyo, kwa Wakristo, hamu yetu ya haki na matendo ambayo yanatokana nayo ni kuchipuka kutokana na upendo wetu kwa Mungu ambaye mwenyewe ni upendo.

Je, ubinadamu wa kuaminika unaweza kuishi kila mara kwa wito huu wa haki kwa sababu ya upendo wetu kwa Mungu? Ndiyo. Yohana 15:9-10anasema: 'Kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. ***10*** Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake.'

Baba, mawazo yako yawe mawazo yangu, mapenzi yako yawe mapenzi yangu, matendo yako yawe matendo yangu, ujasiri wako uwe ujasiri wangu.

**CAROLINE HMINGTHANZUALI**

TERITORI YA INDIA MASHARIKI

Caroline anaishi Aizawl, Mizoram, pamoja na mumewe, K. Zohmingthanga na wana wao wawili (wenye umri wa miaka 12 na 10) na binti (wenye umri wa miaka 7). Yeye ni afisa wa serikali katika Idara ya Ustawi wa Jamii na Masuala ya Kikabila na ana uzoefu katika kufanya kazi dhidi ya watumiaji wa dawa za kulevya, wafanyakazi wa ngono (Makahaba), watu wanaoishi na HIV/UKIMWI, walemavu na raia waandamizi. Yeye ni askari katika kikao cha Aizawl Bazar na ni mjumbe wa Baraza la CHAN (Jumuiya Mtandao wa Hatua za Afya), Mwitikio wa Jeshi la Wokovu kwa masuala ya HIV na biashara haramu ya ulanguzi wa binadamu katika Teritoriya India Mashariki.



## HAKI YA KUENDELEA

LUKA 18:1-8

CATHERINE KAPALO

**'Na Bwana akasema, "Sikilizeni kile mwamuzi asiye na haki anasema. Na Mwenyezi Mungu hataleta uadilifu kwake. Walio mteule, ambao wanamlilia mchana na usiku? Je, ataendelea kuwaondoa? Ninawaambia, ataona kwamba wanapata haki, na haraka. Hata hivyo, wakati Mwana wa Adamu atakapokuja, atapata imani duniani?"'(Luka 18: 6-8).**

Suala la udhalimu wa kijamii sio kitu kipya. Mapambano ya haki ya kijamii yanaweza kufuatiliwa mbali hadi Agano la Kale, kisha wakati wa Yesu na unaendelea hata sasa, hata katika siku zetu za kisasa. Sehemu ya tatizo ni kwamba hakuna mtu anayeachwa kutokana na kupata udhalimu wa kijamii. Sisi sote tumeathirika nayo kwa njia moja au nyingine. Hii ni baadhi ya matokeo ya madhara ya asili yetu ya kuanguka.


Sababu za haki za kijamii zinaweza kutofautiana kulingana na utamaduni na mila, lakini hakuna mtu anayeweza kuepuka kabisa maumivu ya dhulma hizi. Madhara yake hayachukui. Haijalishi unatoka wapi au ni ngozi yako ni gani. Cha kusikitisha, bila kujali ni kiasi gani ulimwengu umejaribu kutetea na kusimamisha tabia hii mbaya, jamii zetu bado zina watu wengi sana walioathirika kwa njia moja au nyingine. Ni kweli kusema kwamba wengi wa waathiriwa wa udhalimu wa kijamii ni wanawake na wasichana, lakini ni wachache tu wanaoweza kuripoti kesi zao wakati wengine wengi hawazungumzii kwa sababu ya hofu au udhibiti mwingine. Watu hawa wanaendelea kuwa kunyamaza, wakiumia na wakati mwingine hufa bila kugunduliwa.

Hili linatuleta kwenye swali la Yesu katika Luka 18: 7-8, 'Wala Mungu hataleta haki kwa wateule wake, ambao mchana na usiku wanamlilia Yeye, ataendelea kuwaondoa? Ninawaambia, ataona kwamba wanapata haki, na haraka.' Hii ni habari njema kwa kweli kwamba Mungu haache waathirika wengi wanao pitia mateso ya kimya ya udhalimu wa kijamii. Lakini kabla ya kuingia ndani zaidi katika utafiti huu juu ya ujumbe wa Yesu katika Luka 18, ni muhimu kwamba tuelewe haki inahusu nini.

## 'HATA KATIKA USO WA MFUMO WA UDHALIMU, HAKI INAWEZA KUFANYIKA.'

Haki ya kijamii ni dhana ya mahusiano ya usawa na ya haki kati ya mtu binafsi na jamii, kama ilivyopimwa na usambazaji ya utajiri, fursa za shughuli za kibinafsi na nafasi za kijamii. Katika Magharibi na pia katika tamaduni za zamani za Asia, dhana ya haki ya kijamii mara nyingi imerejelea mchakato wa kuhakikisha kwamba watu binafsi wanatimiza majukumu yao kwa jamii na kupokea haki yaokutoka kwa jamii. Tunaweza pia kusema kwa urahisi masharti ambayo haki ya kijamii inamaanisha haki na usawa kwa watu wote bila kujali rangi, jinsia, umri, dini, utaifa, elimu, au uwezo wa kiakili au kimwili.

Mungu wetu yuko wazi sana. Anataka watu wake wote wawe kama yeye kwa neno na matendo. Anatutaka sote tuonyeshe tabia yake na kufurahia maisha sawa kama inapaswa kuwa. Hakika yeye ni mfano wetu wa kuigwa kwa ajili ya haki! Katika mfano wa Mjane Mwenye uvumilivu, tunaona kinyume cha Mungu wetu mwenye haki. Tunakutana na hakimu asiye na haki ambaye ameharibika katika utumishi wake, akisita kusikiliza maovu ya mwanamke aliye katika mazingira magumu, mjane. Kazi ya jaji huyu ni kutatua udhalimu – kitu ambacho hafanyi vizuri au kwa hiari – lakini hatimaye anatenda haki kwa sababu ya uvumilivu wa mjane. Mwanamke huyu anasimama dhidi ya ufisadi, akijua kwamba alikuwa na haki na ukweli upande wake. Ikiwa uvumilivu unalipa,



**KUJADILI:**

- Mfano huu unatufundisha nini kuhusu umuhimu wa maombi?
- Soma Luka 18:7-8 tena kwa kulinganisha, labda kutoka kwa tafsiri tofauti za Biblia. Yesu anasema Mungu atafanya au hatafanya nini? Je, hii inatoa onyo gani kwa Wakristo ikiwa tutanyamaza wakati jamii zetu zinateseka kwa udhalimu?
- Orodhesha baadhi ya mifano ya hali ambazo tunahitaji kuruhusu haki kutelemka.

Na hakimu mdhalimu, ni dhamana gani italipwa na Bwana wetu mwenye haki? Mfano huu unatufundisha kwamba hata usoni mwa udhalimu wa kimfumo, haki inaweza kufanywa. Hata hivyo, ni lazima tutambue kwamba ni Mungu pekee anayeweza kuleta haki katika ulimwengu wetu usio wa haki, na sio sisi.

Ni rahisi kuvurugwa kutokana na mapambano yetu dhidi ya udhalimu. Tunaweza kuvutwa kwa urahisi na zawadi nzuri kutoka kwa watu, tunajaribiwa kuwa na wivu kwa nafasi/cheo za juu katika maisha, tunaweza kuwa kiroho pia zaidi ya kusonga pamoja na wengine, na yote haya yanaweza kutuongoza kupuuza mambo muhimu zaidi ya Mungu. Tunaweza kuzidishwa na tamaa, kiburi na ukosefu wa kuridhika ambayo husababisha kuoza kwa maadili na kufa kwa kiroho. Lakini mstari wa kwanza wa Mfano huu (Luka 18:1) unatufundisha kwamba hatupaswi kufa moyo, lakini badala yake tunapaswa kuendelea kutafuta haki daima na 'kuomba daima'. Kama mjane anavyoonyesha katika hadithi yake, uvumilifu hulipa kwa suala la kutafuta kilicho sahihi na cha haki. Tunapovurugwa na ulimwengu unaotuzunguka, na tuwe na raha na ufisadi wake, tunapaswa kujikumbusha juu ya mfano huu.

Kwa Yesu tunaweza kuleta utofauti, kuishi kwa amani na kila mmoja na kufurahia ahadi zake zisizo vunjika milele. Masuala ya haki hushughulikiwa vyema tunapoongozwa na Roho na kutembea katika ukweli na nuru. Hatupaswi kusahau kwamba upendo kwa wengine ni muhimu tunapohudumiana. Tunahitaji kutekeleza ujumbe huu wa upendo na kuuishi tunapojitahidi kukabiliana na udhalimu. Tunapaswa kuwa watu ambao wanaweza kutembea na kusema - tukijua kwamba Mungu yuko upande wetu, na kwamba anafurahi na wale wanaosikia na kuweka vitu katika mazoezi.

Mpendwa Mungu, kutuwezesha na kutusaidia kwa Roho wako kuwa wafuasi wa Kristo ambao wanaweza kutekeleza haki Katika dunia hii. Tusaidie kuchukua taarifa ya wale wanaotukaribia kwa msaada na kutusamehe kwa kugeuka migongo yetu juu yao wakati tungewakaribisha badala yake. Katika jina la Yesu tunaomba, Amina.


## CATHERINE KAPALO

### TERITORI YA MALAWI


Bi Catherine Kapalo ni Mkina Wokovu ambaye hutumika kama Sajin Meja (CSM) katika kikao cha Lilongwe. Catherine anafanya kazi katika idara ya Ukatili wa Kijinsia na Sera ya Jumuiya ya Haki za Binadamu na Mratibu wa Serikali ya Malawi. Alikuwa mwanamke wa kwanza kudhaminiwa na serikali ya Malawi kufuatilia masomo yake ya uhandisi nchini India.



# KUPITIA MACHO YA MUNGU

MITHALI 31:8-9

MEJA KAREN ETCHEVERRY

**'Fumbua kinywa chako kwa ajili yake aliye bubu; Uwatetee watu wote walioachwa peke yao; *9* Fumbua kinywa chako, uhukumu kwa haki; Uwapatie maskini na wahitaji haki yao.' (Mithali 31: 8-9).**

Ninaposoma kifungu hiki cha Maandiko na swali: kwa nini tunaulizwa kuzungumza kwa wale ambao hawawezi kuzungumza kwa ajili yao wenyewe? Kwa nini ni muhimu? Kwa nini tuagiziwe kufanya hivyo? Kwa nini hatupewi uchaguzi? Pengine kwa sababu sio kawaida kusimama kwa niaba ya wale walio na mahitaji zaidi.

Angalia picha hii, iliyochorwa na William Ely Hill mwaka 1915. Unaona nani? Unaona mwanamke, kijana au mzee? Anafananaje? Je, unaweza kuona yote mbili? Naam, jibu lolote ni sahihi! Yote inategemea na mtazamo wako na jinsi unavyo itazama hii picha.

**'NI JUU YETU KUPATA VITU VIDOGO TUNAVYOWEZA KUFANYA AMBAVYO VITACHANGIA MABADILIKO MAKUBWA ZAIDI.'**


Sasa, jiulize: Unawaangaliaje wengine? Kwa macho, ile ingine ni tofauti na kwa hivyo inanidhoofisha. Yote inagharimu tu mwingine rangi ya ngozi, safari ya maisha, usemi, tabia, kwa mtu mwingine kuonekana kama chukizo, madhara, au mtu aogopwe na kukimbia.

Hebu tufikirie jinsi Mungu anavyotuona sote, bila kujali ya vitu vinavyotugawanya. Mtazamo wa Mungu kwetu ni wa kupendeza. Mungu hutazama kila mmoja wa viumbe kvyake wa njia ambayo hakuna kitu kinachoweza kubadilisha. Kila kiumbe ni sehemu ya mpango wake na 'Mungu aliona kwamba ilikuwa nzuri sana' (Mwanzo 1:31).

Ili kuwatendea watu haki, lazima ubadilishe jinsi unavyowaona. Ni hivyo rahisi. Ninapomwona mtu nakumchukulia mzee, au mpwekee, au maskini, au wenye mahitaji, au mnyonge na mchovu, Mungu anamwona mtu huyo huyo kama kijana, tajiri, wa thamani, na wa maana sana! Lazima nitafute uzuri wa Mungu katika kila mtu. Lazima nitafuta kuangalia mtu mwingine kwa macho ya Mungu, kuona upendo wa Mungu kwao kwanza. Kisha sioni tena Mithali 31:8-9 kama utaratibu, lakini kutambua kwamba nina mtazamo wa haki sawa na Mungu!

Mistari hii ya Mithali inaniongoza kuhisi huruma ile ile Yesu alihisi. Inakuwa na nguvu sana kwamba huna njia mbadala lakini kuzungumza kwa niaba ya wengine. Na hatimaye, jambo lisilo la kawaida kwako kufanya, linakuwa desturi yako. Bila shaka, bado utalazimika kukabiliana na hofu yako, kuacha mahali pako pa usalama, na kujihatarisha. Haya yote yanahitaji ujasiri, lakini yanaweza kufanywa kwa msaada wa Mungu. Ni juu yetu kufanya mambo madogo madogoambayo huchangia mabadiliko makubwa.

Nikikumbuka mambo ya kikao chetu cha Strasbourg, Ufaransa, ningependa kushiriki hadithi chache za Maisha kuhusu watu watatu waliopokea huduma zetu, 'G', 'M' na 'N' ambao walikataa kukubaliana na huduma yetu. Waliishia mtaani na hakuna aliyetaka kuwatetea. Walikuwa wenye mahitaji sana, hawajua kuzungumza lugha yetu wala hawakufanya jitihada ya kujaribu kuongea. Pia walikuwa na wazimu kwa huduma yoyote ya utawala, ambayo ilisababisha hali ngumu katika kuwasaidia. Baada ya miezi kadhaa ya kujuana na kufanya kazi mbalimbali za huduma za kijamii, tuliweza kutathmini haki yao ya malipo ya uzeeni. Ilikuwa safari ndefu, ya upinzani mkubwa, lakini hatimaye ulikuwa na matunda. Tulisimama kwa niaba yao na kuwatetea.



**KUJADILI:**

- Fikiria mtu asiye na furaha na maskini. Unawaangalia vipi? Mungu anamwonaje?
- Katika mtaa wako, ujirani na kanisa, ni nani unaweza kutetea? Jinsi gani?
- Kanisa lako lingesema nini au lingeendelea kuongea na mamlaka kwa niaba ya asiye bahatika na maskini?



Drawing by the cartoonist William Ely Hill, 1915, public domain

Katika tukio lingine, familia ya 'L' baada ya kupata haki yao kisheria walihitaji nyumba ya ghorofa. Hawakujua lugha ya wenyeji vizuri mbala na kuwa na rasilimali chache. Mkina wokovu aliwaongoza katika hatua hizi, kuangalia matangazo magazetini kila siku, kuwaandamana nao kutazama nyumba za ghorofa, kuwasaidia kujaza nyaraka, kuwa mdhamini wao, na hata kusaidia kulipa malipo ya kwanza (amana). Aliongea kwa niaba yao, kwa sababu hawakuweza kujizungumzia wenyewe.

Kwa 'L na S' ilikuwa rahisi sana. Tuliwajua vizuri kibinafsi kupitia kazi yao ya kujitolea katika Kikao kwa zaidi ya miaka mbili. Walipoomba kazi zao za kwanza, tuliwasimamia kila mmoja wao nakushuhudia ufanisi, kuwa watu wa kuegemewa na thamani yao.

'V' ni mtu mzee ambaye hana familia. Tulishughulikia taratibu zote za kiutawala kwa ajili ya kustaafu na kuelekea nyumbani kwake, lakini pia ilikuwa muhimu kusaidia bajeti yake, msaada kijamii na kufanya mawasiliano na benki yake. Tulimtetea alipokuwa ameachwa.

Sio njia rahisi, na mara nyingi ninahitaji kurudi kwenye fungu hili. Inanikumbusha maneno muhimu ya haki wanayohitaji wasio bahatika na maskini. Neno la mtu mmoja linatosha kubadili jinsi mwathirika anavyohisi kwa undani kabisa. Hata mbele ya umati wa watu, inatosha kwa mtu kusema kwamba hali hii si haki kwa mwathirika kuhisi huyuko peke yake. Tunaweza kuwa sauti hiyo ya huruma na haki.



Mungu, niruzuku ili niweze kutamka hukumu sawa na wewe; nipe akili yako ya haki. Wakati ninapaswa kuwahukumu maskini, acha niwe mtiifu na waaminifu kwa sheria. Na milima ikawepe amani, na vilima haki' (Zaburi 72: 1-3).

## MEJA KAREN ETCHEVERRY

### TERITORI YA UFARANSA NA UBELGIJI



Meja Karen Etcheverry ni afisa wa Kikao cha Strasbourg akiwa na mumewe Joel. Wazazi wake walikuwa maafisa, lakini kukubali kwamba Bwana alikuwa anamwita awe afisa haikuwa rahisi. Hata hivyo, tangu wakati alipojiachilia na kukubali njia ya Mungu, nafsi yake yote iliguswa na amani ikamjia. Miaka ishirini na tano baadaye, amani hii bado ipo na humsaidia kuishi kila siku, siku nzuri na siku ngumu zaidi.

# NENO LETU, MIENENDO YETU NA KAZI YETU

YAKOBO 1:19–2:26

MEJA SHARI RUSSELL

**‘Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.’ (Yakobo 1:27).**


Kama Wakristo tuna fursa ya ajabu na mwito wa kuwa sehemu ya kazi ya Mungu ulimwenguni. Yuko kazini katika maisha yetu na jamii zetu; kwa wanyonge na wenye nguvu. Mwito wetu ni kujiunga na kazi yake na kudhihirisha neema yake, maadili na utakatifu kwa ulimwengu uliopotoka. Somo letu kutoka Yakobo linatambua njia tatu ambazo sisi tunaweza kuishi wito huu: kupitia neno letu, kutembea kwetu na kazi yetu.

Kwanza, hebu tuangalie 'neno letu'. Yakobo 1:19-20 inaanza na ukumbusho wa jinsi maneno yetu yanavyoathiri ushahidi wetu. Yakobo anashiriki sheria tatu za maisha: Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika; Katika Yakobo 1:22-24, tunapata tofauti kati ya wale wanao sikia neon tu na wale wanao sikia na kutii. Katika mstari wa 23 neno 'angalia' (katanoeō) linamaanisha fikiria kwa makini, na katika mstari wa 25 neno kwa 'kuangalia kwa makini' (parkypto) inamaanisha kuchunguaza kwa udani. Maneno yote mawili yana maana sawa. Wala haimaanishi mtazamo wa kupita. Hii kulinganisha basi ni juu ya athari za kutazama ambazo ni kusahau au kutii na kuendelea katika Neno. Neno 'halina maana' (linalopatikana katika Yakobo 1:26) linamaanisha kisicho na nguvu, kweli, matokeo; haina maana, bila kusudi. Inawezaje kutodhibiti ulimi wetu kutoa ushuhuda usio na maana? Je, Yakobo 2:12 na Yakobo 3:1-12 anaendelea kusema nini kuhusu maneno yetu na hotuba?

**‘HATUTAJUA KILE MUNGU ANAHITAJI KUTOKA KWETU KAMA HATUWEZI TEMBEA PAMOJA NAYE NA KAMA HATUJAUNGANISHWA NAYE KIROHO.’**

Pili, hebu tuangalie 'mienendo yetu'. Yakobo 1:21-25 inatukumbusha tujiangalie wenyewe kwa uaminifu sehemu zilizofichwa za maisha yetu. Amri ya 'kukubali neno lililopandwa ndani yako' linakukabalika tu na msemo 'kwa unyenyekevu'. Yohana 1 inatukumbusha 'neno' inajumuisha zaidi ya mistari yaliyoandikwa. Je, ni vikwazo gani vinaweza kutuzuia kukubali kikamilifu neno kwa unyenyekevu? La muhimu ni kuvua na kuacha uchafu wote, Yote wawili ni matendo ya makusudi kwa Wakristo: kukubali Neno huku tukikataa uovu. Taswira ya kuacha uchafu wote inapatikana katika Zakaria 3 ambapo Kuhani Mkuu, ambaye anawakilisha taifa lote, yuko katika mavazi machafu yaliyorarukararuka.

Yakobo 1:27 inalinganisha na dini isiyo na maana na mwelekeo na dini safi na isiyo na mawaa. Mstari wa 26 inawapa changamoto wale ambao wanaweza kutafuta baraka kwa sababu ya matendo yao ya kidini au tabia yao. Tunawezaje kujaribiwa kutafuta baraka kupitia tabia zetu? Neno 'safi' halimaanisha tu usafi wa vitu vya kidini bali pia kutakasa moyo. Neno 'lisilo na taka’ linamaanisha kuwa huru kutokana na uchafu au kasoro. Sentensi ya Kigiriki, inaanza na safi na isiyotiwa taka kumaanisha dini na kumalizia kwa mwito wa kujikinga kutokana na kuchafuliwa na ulimwengu. Neno 'cosmos' (ulimwengu) linaunganishwa na neno ‘cosmetic’ kumaanisha 'kupanga kitu' au kujiangalia uso'. Yakobo anafafanua kwamba kujua ulimwengu ni kumwacha Mungu nje.



**KUJADILI:**

- Je, changamoto tunazokumbana nazo, ni zipi zinaonyesha uhusiano kati ya imani na matendo?
- Ni nini umuhimu na athari za 'safi na isiyo na taka' inayofuatana na 'dini' yetu katika maisha yetu ya kila siku?
- Katika muktadha wetu sasa, tunawezaje kudumisha mifumo ya udhalimu na ukandamizaji badala ya kutafuta haki na uhuru?

Hatimaye, hebu tuangalie kazi yetu. Kuwa sehemu ya kazi ya Mungu inamaanisha kuwaona wengine kama Mungu anavyowaona, hasa wale hawana chochote cha kurudisha mkono. Hii inapaswa kuwa dhahiri katika huruma yetu kwa wale wasiyobahatika. Yakobo anatumia maneno 'mjane na yatima' kuwaakilisha wote wenye kutengwa au kudhulumiwa.

Kote katika Yakobo 2: 1-7, suala la upendeleo na mamlaka na nafasiza juu yamedadiliwa. Matajiri walikuwa wamewekandamiza waumini wa kwanza lakini badala ya kuwalipiza kisasi, hatari ya kuwaridhisha au kuwatetea matajiri ilisababisha chuki dhidi ya maskini. ‘Kuegemea upande’ inahusu kufanya hukumu au tofauti kulingana na sifa kama sura, jinsia, kabila au hali ya maisha. Badala ya kupinga mifumo ya ukandamizaji, walikuwa wanatoa heshima kwa wale wanaojihusisha kikamilifu katika kuwakandamiza wengine kupitia kwa uchumi. William Booth, alipogundua kuwa Kanisa la Methodisti limekuwa 'linaheshimika sana', alitafuta kudumisha mwito wake kwa wale waliokuwa katika mazingira magumu zaidi na waliopuuzwa na kanisa. Jeshi la Wokovu linawezaje kujibu hatari hii leo ya kuwa na heshima sana na kuwatetea wale wenye uwezo na upendeleo?

Katika Yakobo 2: 8-13, Yakobo anatarajia kuwa wengine wanaweza kutetea upendeleo wao kwa matajiri na kusema kuwa wanatimiza amri ya kumpenda jirani yao. 'Kuonyesha upendeleo' kunaweza kuwa dhambi vipi? Katika mistari ya 14-26, Yakobo haendi kinyume na Paulo lakini anazingatia imani yetu baada ya wokovu. Kutumia mifano ya Ibrahimu (Baba Mkuu wa Kiyahudi) na Rahab (mwanamke wa mataifa mwenye maisha kutilia maswali), Yakobo hapingi tu tabia ya kuegemea upande inayo iliyo Kanisani bali anawakilisha mambo mawili tofauti iyodhihirisha imani yetu. Je. Ni kanuni gani tuzionazo katika kwa mifano hii miwili ambazo tunaweza kuiga katika maisha yetu?



Asante, Bwana, kwa fursa na wito wa kuwa sehemu ya kazi yako ya kubadilisha ulimwengu wetu.
Na tuweze kutafuta kweli na upendo kwa ujasiri mioyoni mwetu na kuwa vyombo vya neema yako na minara ya tumaini tunapotafuta haki na uhuru kwa wote.


**MEJA SHARI RUSSELL**

TERITORI YA KANADA NA BERMUDA




Meja Shari Russell ni Muanishinaabe (Saulteaux) na ameolewa na Robert. Pamoja, wana watoto watatu wazuri: Charles, Gavin na Brannon. Waliagizwa kama Waombezi Waaminifu mwaka 1999 na wamekuwa na maagizo katika vikao mbalimbali na Chuo cha Mafunzo ya maafisa. Shari alikamilisha BA yake na MA katika Masomo ya Kibiblia na Theolojia na kwa sasa anaendeleza PhD na NAIITS kupitia Chuo Kikuu cha Uungu (Melbourne). Hivi sasa, Shari hutumika kama Mshauri wa Wizara za Asili wa Teritori ya Canada na Bermuda.

# HAKI TOKA MOYONI

MICAH 6:1-8

KAYLEEN SAM

**‘Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako!’ (mstari wa 8).**

Kitabu cha Micah kinahusu hukumu ya Mungu juu ya Israeli. Israeli ilipuuza amri za Mungu na kuanza kuabudu miungu mingine. Hata kama walimtolea Mungudhabihu na sadaka kudhibitisha ibada yao, mioyo yao haikuunganika na Mungu wala kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu. Mungu alijua mioyo yao ilikuwa mbali naye naye akatamani waweze kumrudi kwake tena. Tunaposoma Mika tunaanza kuelewa kwamba haifai kupoteza uhusiano wetu wa binafsi na Mungu.


Mungu anahitaji mambo mengi kutoka kwetu lakini la muhimu zaidi ya yote ni uhusiano wetu wa binafsi naye; kutembea kwa unyenyekevu na Mungu. Ikiwa tunatamani kujua kile Mungu anasema na kumjua zaidi, basi lazima kuwa na uhusiano wa karibu na wa kibinafsi naye. Lazima tumtafute kila siku, kulishwa neno lake na kuwasiliana naye kwa njia ya maombi. Hatutajua kile Ambacho Mungu anahitaji kutoka kwetu ikiwa hatutatembea na yeye na hatujaunganishwa kiroho naye. Kuunganishwa huleta mawasiliano. Roho zetu lazima ziunganishwe kwa roho ya Mungu, mioyo yetu lazima iunganishwe na moyo wake na tunapomkaribia, naye atatukaribia (Yakobo 4:8).

Sisi ni mikono na miguu ya Mungu, na ili mikono na miguu ya Mungu kusonga duniani lazima tufungue mioyo yetu kumwalika akatembee ndani yetu. Mika anawauliza watu wa Israeli kuhusu aina ya dhabihu ambayo Mungu ankataka kutoka kwao: ‘Nimkaribie Bwana na kitu gani, na kuinama mbele za Mungu aliye juu? Je! Nimkaribie na sadaka za kuteketezwa, na ndama za umri wa mwaka mmoja? ***7*** Je! Bwana atapendezwa na elfu za kondoo waume, au na elfu kumi za mito ya mafuta? Je! Nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza kwa kosa langu, mzao wa mwili wangu kwa dhambi ya roho yangu?’
(Micah 6:6-7).

**'ROHO ZETU LAZIMA ZIUNGANISHWE NA ROHO YA MUNGU, MIOYO YETU LAZIMA IUNGANISHWE NA MOYO WAKE NASI TUMKARIBIE MUNGU.’**

Mungu hapendezwi na aina nyingine za dhabihu. Mungu hupendezwa tunapojitoa sisi wenyewe kama dhabihu iliyo hai kwake, takatifu na kutengwa kwa ajili ya mapenzi yake. Mungu hawezi kufanya kazi peke yake;
anahitaji watu ambao wako tayari kujitoa kabisa kwa ajili ya wale wanaoteseka na waliopotea. Tunapokuwa na mizizi imara na kunganishwa na Mungu, basi kila kitu ambacho Mungu anahitaji kutoka kwetu kinaweza kufunuliwa (Watu wabaya hawaelewi na hukumu; Bali wamtafutao Bwana huelewa na yote. Mithali 28:5).

Njia za Mungu ziko juu kuliko njia zetu, mawazo yake yako juu kuliko yetu (Isaya 55:9) na kwa hivyo haki ya Mungu ni tofauti kabisa na mtazamo wa haki yaulimwengu. Haki ya Mungu sio kile tunachofanya kutoka nje, lakini ndicho kinachotoka ndani ya mioyo yetu. Haki ya Mungu sio tu jambo ya kawaida kufanywa wakati wowote kuna wito. Inapokuwa jambo la kawaida, la kila siku, sisi polepole huanza kupoteza mwelekeo wa umuhimu wetu wa kumkaribia kwanza. Katika mistari ya sita na saba, Micah anapendekeza kwamba wakati dhabihu zilikuwa jambo la kila siku, walianza kupoteza mwelekeo wa sababu ya kutoa dhabihu. Shughuli zilipoteza maana na kuwa tu maonyesho bila uzito, na ikawa si matendo ya kweli ya kuabudu kutoka moyoni. Ni upendo tu huleta uzito.



**KUJADILI:**

- Je, Mungu anahitaji nini kutoka kwako kutafuta haki?
- Unawezaje kuwa mikono na miguu ya Mungu (Ni dhabihu gani utakayofanya ili kumpa Mungu)?
- Unawezaje kuonyesha upendo wa Mungu (Ni matendo gani au shughuli gani unazofanya zinaonyesha upendo wa Mungu)?

Upendo ni kiini cha haki ya Mungu na ni nguvu yenye sumaku. Wakati mioyo yetu inaunganika na Mungu, tuna kuwa njia ya upendo wake usiokoma, kuisambaza kwa wale ambao wanaihitaji sana.

Haki ya kijamii ni upendo katika matendo, tukiwatambua wanaoumia na kuhisi maumivu yao kana kwamba ni yetu wenyewe, na wanasukumwa kupona na kuhuhishwa katika jina la Yesu. Lakini tendo bila upendo haimaanishi chochote kama mioyo wetu sio sawa na Mungu.

Mungu anataka haki yake kujidhihirisha ndani yetu tu wakati dhabihu zetu ni za kutoka moyoni. Kutembea kwa unyenyekevu na Mungu inatufanya kuwa mikono na miguu ya Mungu, na kutufanya kuwa njia ya upendo wa Mungu, inayotiririka na kuwafikia wale wanaoteseka. Hebu tuonyeshe ulimwengu Mungu ni nani na kuwa mshale unaoonyesha njia ya kurudi kwa Mungu.



Mungu wangu, Baba yangu, nifundishe jinsi ya kuvuta moyo wangu karibu nawe; kwa njia ya maombi na kutafakari katika Neno lako, kunisaidia kujenga uhusiano huu wa kibinafsi na wewe kwanza, kabla sijafikia wengine wanaohitaji upendo wako kwa haki yako. Amina.

## KAYLEEN SAM

### TERITORI YA PAPUA GUINEA MPYA NA VISIWA VYA SULEIMANI

Kayleen ni mwalimu wa shule ya sekondari katika Jimbo la Nyanda za Juu Mashariki jimbo la Papua Guinea Mpya na anaunga mkono kikao chake huko Goroka. Hapo awali alifanya kazi katika Jeshi la Wokovu katika Tume ya Kimataifa ya Haki za Kijamii mjini New York, Marekani.



# UKARIMU NA UTAKATIFU

LUKA 11:37-52

KAMISHNA JANE PAONE

**Akasema: Yesu akajibu, "Nanyi wataalamu katika sheria, ole wenu, kwa sababu mmewapakia watu mizigo hamwezi kubeba, na ninyi wenyewe hamtainua kidole kimoja ili kuwasaidia" (Luka 11:46).**


Tunatamani kumsikia Yesu akiongea maneno ya faraja, lakini hapa anasema, 'Ole wako!' kwa makundi mawili ya uongozi wenye ushawishi katika jumuiya ya Kiyahudi. Mafarisayo na wataalamu wa Sheria walikuwa na jukumu la kujifunza Sheria ya Musa na kuitumia kila siku. Mafarisayo waliendele utaratibu waTorati wakati wa shida baada ya uharibifu wa pili wa hekalu. Shukrani kwao, masinagogi yalishamiri na sura ya Kiyahudi ikaendelea kuonekana.

Mmoja wao alimsikiliza Yesu akifundisha na kuthubutu kumwalika Yesu aliyekuwa na sifa ya kula na wenye dhambi, nyumbani kwake.
Luka ana hadithi kadhaa za ukarimu ambapo Yesu alikuwa mwenyeji au mgeni na alifurahia chakula na ushirika. Hata hivyo, katika tendo rahisi, la la kukaa chini kila siku na kushiriki chakula na wengine, alifanikiwa kuamsha fujo! Ofa hii ya ukarimu ilikuwa na masharti yaliyoambatana nayo.
Yesu alitarajiwa kutekeleza utakaso wa kidini ambao Mafarisayo walitekeleza na kutaka wengine kufuata: kule kunawa mikono ili kuwa ishara kutakasa uchafu wa kitu chochote walichokuwa wamegusa, kuzuia uchafusi. Watu, wenye shauku ya kuishi maisha yaliyompendeza Mungu, 'kutenganishwa' na 'wasio waaminifu', kwa kuwa waliamini wenyewe ni wasafi. Yesu alithubutu kukiuka mila yao ngumu!

**'YESU HAKUWEZA KUBAKI KUTOKUWA NA UPANDE WOWOTE, NA HATUWEZIKUBAKI KUTOKUWA NA UPANDE WOWOTE KUHUSU UHAKIKA WA MASUALA AIDHA.'**

Kama ilivyo katika tukio lingine wakati wa huduma yake ya kuleta haki duniani, Yesu anmnuku nabii Isaya (10: 1-2). Maneno yake makali kwa Mafarisayo na wataalamu katika sheria, ambao, walizingatia majukumu yao ya kidini, lakini bado walipuuza furaha ya kuwa pamoja naye. Wakitamani kufanya kilicho sahihi, walisahau kuwa na uhusiano sahihi: Upendo kwa Mungu na kwa wengine ilikamilisha zile amri. Nia ya kuwa watakatifu, wakasahau kuwa wakarimu kwa kuwaonyesha wengine wema na huruma. Kwa mitazamo na matendo yao, kutenga badala ya kuingiza kukawa matokeo. Walihukumu, wakapenda sifa, hawakuwa na ufahamu wa wao kukosa usafi wao wa ndani kwa sababu waliwaza tu yawalivyoonekana kwa nje. Waliwazuia wengine kujifunza kuhusu ufalme wa Mungu wa haki; walikandamiza na kutumia vibaya uwezo wao.

Yesu hakuweza kubaki bila upande wa kuunga mkono, nasi hatuwezi kubaki bila upande wowote kuhusu masuala fulani aidha. Dhambi za ukandamizaji huwaahuathiri wanaokandmizwa na wenye kukandamizwa. Desmond Tutu anasema kuwa watu wa nje hawapaswi kuwa lengo la ubaguzi la vis-vis apartheid Afrika Kusini. Anafafanua kuwa msimamo kama huu ni kama: 'Faraja kwa panya ambaye ndofu amesimama juu ya mkia wake na kusema, "Mimi sina upendeleo". Katika mfano huu, unaunga mkono sana ndofu katika ukatili wake. Kwa mtaalamu katika sheria ambaye alilalamika kwamba Yesu alikuwa akiwashutumu wao pia, Yesu akasema: ‘Nanyi wana-sehria, ole wenu, kwa sababu mwawatwika watu mizigo isiyochukulika, wala ninyi wenyewehamwigusi mizigo hiyo hata kwa kimoja cha vidole vyenu ili kuwasaidia' (Luka 11:46).



**KUJADILI:**

- Kwa nini unafikiri maneno ya Yesu kwa wataalamu wa sheria yalikuwa makali sana? Fikiria matokeo ninnini kwa sababu ya matendo yao, na maneno ya Yesu?
- Tunafumbuaje maneno ya Yesu ya haki thabiti na huruma kwa wanawake na wengine ambao wanaweza kuhisi Kutengwa?
- Mfarisayo ameelewaje ukarimu na utakatifu? Fikiria kuhusu wale tunaowaalika katika nyumba zetu na jinsi tunavyowatendea. Kumbuka kwamba ukarimu wa kweli, ni kama utakatifu, ni kitendo cha ukarimu wa neema.

Mizigo ya ibada za kisheria ambazo wataalamu wa sheria walioweka kwa watu huenda zilikuwa nzito, lakini kutojali kwa jinsi sheria hiyo ilivyotekelezwa, na watu wenye tabia zisisoenda na sheria, ilifanya sharia kuwa nzito zaidi! Watu hawa walipaswa kuwavutia watu kwa Neno la Mungu lakini badala yake waliwafungia nira nzito (Matendo 15:10). Haya yatakuwa na matokeo ya milele: watawajibika. Mtazamo wao wa hukumu uliowekwa unaashiria sheria bila upendo. Hawagusi hata mizigo hiyo kwa kutumia vidole vyao ili kupunguza maumivu ya wengine waliowekewa mizigo. Neno hili la Kiyunani linatumika hapa tu katika Agano Jipya, neno la matibabu la kiufundi la kugusa, linalotumika wakati daktari anahisi sehemu za maumivu ya mwili katika jaribio la kupunguza uchungu. Wataalamu wa sheria wangesaidia, lakini hawakufanya hivyo.

Kinyume na hayo, Yule aliye upendo anaalika kila mmoja wetu: 'Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi' (Mathayo 11:28-30).



Bwana, nisaidie kutembea kwa haki, na moyo safi, wenye upendo - kwa ukarimu kutoa upendo niliopokea kutoka kwako ili nisihukumu, lakini nimwona Kristo katika kila mtu ninayekutana naye.


**KAMISHNA JANE PAONE**

TERRITORI YA UINGEREZA NA JAMHURI YA IRELAND


Anajivunia asili yake ya Uskoti, Kamishna Jane Paone ametumika katika Jeshi la Wokovu kama afisa, pamoja na mumewe Massimo, nchini Uingereza, Ufaransa, Italia na Uswisi, wamekuwa viongozi wa teritori ya Italia na Ugiriki, Ufaransa na Ubelgiji na Uswisi, Austria na Hungari. Alikuwa sehemu ya Tume ya Kimataifa ya Sheria ya Jamii hadi alipostaafu. Jane alikuwa msemaji juu ya haki ya kijamii katika Bunge la Boundless, na katika mkutano wa utakatifu wa kijamii nchini Haiti na Kanada. Anaendelea kuwa na shauku ya kupigania haki katika Jeshi na ulimwengu mzima, kwa lengo la kuunganisha vizazi vyote na jamii ili kuleta matokeo halisi kwa matendo makuu.



## MPENDe JIRANI YAKO KAMA UNAVYOJIPENDA MWENYEWE

MATHAYO 22:34-40

MEJA COLLEEN HUKE

Mistari yetu ya Biblia inaanza na Yesu kuwa lengo tena kwa mashambulizi ya viongozi wa kidini! Katika

Ujumbe wa tafsiri ya Mathayo 22, tunasoma kwamba 'wakafanya shauri pamoja jinsi ya kumtega kwa maneno', lakini mapema tulihakikishiwa kwamba Yesu alikuwa tayari ametambua nia zao. Wakati Yesu alipovamiwa kwa swali 'katika torati ni amri ipi iliyo kuu?', jibu lake lilisababisha utata uliotarajiwa kwa sababu kulikuwa na amri 613 katika sheria ya Kiyahudi - mengi yao yakianza kwa 'usifanye' - na zote zilizingatiwa kuwa na umuhimu sawa.


Jibu la Yesu kwao linasisitiza kwamba ingawa wanatii maandiko ya sheria, jambo kubwa ni kuelewa madhumuni ya sheria ambayo hatimaye na daima huwa upendo. Akasema: Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote." Hii ni amri ya kwanza na kuu. Na ya pili ni kama hili: "Mpende jirani yako kama nafsi yako."' Yesu anaweka wazi kwa Mafarisayo walioishi kisheria - kama vile anavyotuambia leo - kwamba hakuna kitu muhimu zaidi ya kumpenda Mungu na kupendana.

**'Kama hatutaona Kristo kwa wengine na kuwapenda kwa upendo wa Mungu, hawataona Kristo ndani yetu.'**

Utiifu kwa amri hizi mara mbili ni kiini cha injili, msingi wa kazi ya Jeshi la Wokovu na inapaswa kuwa mzizi wa matendo yote ya kijamii ya Kikristo na haki. Wajibu wetu wa kijamii hauwezi kubadilishwa kwa utimilifu wa majukumu na mila za kidini. Yesu anapoendelea kuwaelekeza viongozi wa kidini: 'Ole wenu, walimu wa sheria na Mafarisayo, ninyi wanafiki!... Mmepuuza mambo muhimu zaidi... haki, rehema na uaminifu' (Mathayo 23:23). Yesu anaonekana kusema kwamba hatuwezi kumpenda Mungu na vitu vyetu vyote bila kumpenda jirani yetu, na hatuwezi kumpenda jirani yetu bila kumpenda Mungu.

Kinyume na tafsiri maarufu, kumpenda jirani yako 'kama nafsi yako' hairejelei picha ya kibinafsi, badala yake ni kutambua sura ya Mungu katika watu wote. Kwa njia hii, tunapompata Mungu katika wanadamu wenzetu, tunaona watu wote kama ndugu na dada zetu, walioumbwa kwa mfano wake, wanaostahili kutendewa usawa na haki bila ubaguzi. Matendo yetu lazima yahakiki Mathayo 7:12: 'Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii.' Katika maneno mengine, lazima tumtendee jirani yetu kama vile tungelipenda kutendewa, na wakati jirani yetu anatendewa vibaya, lazima tuwe sauti inayotetea heshima ya binadamu na haki ya kijamii kwa niaba yao.

Ikiwa hatutaona Kristo kwa wengine na kuwapenda kwa upendo wa Mungu, kamwe hawataona Kristo ndani yetu. Ni upendo wake Mungu tu ambao unatuwezesha kuwapenda wanadamu wote bila ubaguzi na kuwatendea wote kwa heshima, hasa maskini, wanaokandamizwa na wasio bahatika katika jamii.
Katika Mathayo 25:40, Yesu asema kuwa chochote tulichowatendea mmoja wa ndugu na dada zetu, kwa kweli tulikuwa tukimtendea yeye. Mama Teresa wa Calcutta alirejelea hili aliposema: 'Mwisho wa maisha hatutahukumiwa na idadi ya diploma tumepokea, kiwango cha fedha tulizotengeneza, makubwa tuliyoyafanya. Ila tutahukumiwa kwa "Mimi nilikuwa na njaa na ulinipa kitu cha kula, nilikuwa uchi na ulinivika, sikuwa na makazi, na mkanikaribisha."



**KUJADILI:**

- Je, 'Kuwapenda wengine' unaonekanaje kwako?
- Fikiria ubaguzi wako mwenyewe na / au hisia za kibinafsi. Kwa njia gani hili linaweza kushawishi matumizi ya amri ya Mungu katika Mathayo 22:39?
- Unawezaje kutetea huruma na haki kwa niaba ya mtu unayemjua aliye katika haja ya upendo usio na ubinafsi na usio na masharti sasa hivi?

Ni muhimu kuelewa maana ya upendo katika mistari hii. Haihusiani na hisia kali, tunavyoelewa upendo kwa kawaida. Neno la Kiyunani linalotumika kwa upendo sio falsafa ambalo linaonyesha hisia za kupendeza na upendo wa kirafiki, lakini “Agape” ambayo inaonyeshwa vizuri kwa fadhili za upendo. Ufafanuzi wangu ninaoupenda fadhili za upendo ni 'rehema tekelezi' na ninayoihisi kila siku katika uhusiano wangu na Mungu. Ananitendea mimi upendo usio na masharti, rehema na huruma; kupewa kwa ukarimu na kwa uaminifu, bila kujali jinsi ninavyostahili! Hata hivyo, Wakristo wengi wanashikilia mitazamo na nia ambayo inawafanya wanyime jirani wao upendo. Matendo yao mara nyingi hutegemea hisia za kibinafsi kwa rafiki au adui pamoja na chuki kuhusu jinsia, umri, rangi, makabila, dini, ulemavu au elimu; na jinsi wanavyo waamini, jirani kuwa katika mwanga wa hali hiyo.

Hata hivyo, upendo ulioamriwa katika Mathayo 22:38-39 haiathiriwi na hisia, chuki au hadhi. Tunahitaji kutazamia tu Msalaba kwa uthibitisho. Yesu alionyesha 'rehema tekelezi' alipoonyesha upendo wa “Agape”. Upendowa kuokoa ulimwengu uliomdharau na kumkataa. Msalaba ulikuwa ni kitendo cha mapenzi, uamuzi uliopaswa kufanya, ilikuwa upendo wa kihisia kwa wanadamu wote. Mwili wa Kristo lazima ushiriki aina hii ya upendo huu wa kutobaguwa na usio na masharti kwa wanadamu wanaoumia katikati ya udhalimu unaokua unaposukumwa na hisia za huruma, lakini pia wakati sivyo. Lazima tukusudie kufanya maamuzi ya mapenzi kila siku ili kuleta ufalme wa Mungu duniani, kwa kuonyesha rehema tekelezi bila ubaguzi kwa jina la Yesu. Sio hisia za upendo ulioamriwa, lakini kuchagua kuwapenda wengine kutokana upendo wa Mungu usio na masharti kwetu na kama kujieleza upendo wetu kwake.

Ni rahisi kutilia shaka uwezo wetu wa kuleta mabadiliko tunapozingatia dhulma zote za kijamii zilizoenea katika jamii zetu duniani kote, hasa kuhusiana na wanawake na wasichana wadogo. Hata hivyo, maoni ya Biblia yanabainisha kuwa Wayahudi kwa kawaida walitafsiri 'jirani' kama 'mtu aliye karibu'. Kwa hiyo, amri ya Yesu kumpenda jirani yako anatuita kutenda mema kwa maslahi ya wale walio karibu nasi. Wakati hurumia wa Yesu msalabani ilibadilisha matarajio yetu sote, mistari hii inaashiria kwamba lazima tuanze kuishi kwa huruma na haki pale tulipo.

Ninapenda dhana kwamba 'haki ni upendo kutafsiriwa katika sera za kijamii' kwa sababu inapendekeza kwamba wakati tunatakikana kuleta mabadiliko ya kijamii, hapo ndipo upendo unapoanza. Yesu anadumisha kwamba mafundisho yote ya kidini yanategemea na yanatimizwa kwa neno moja tu: Upendo.



Mpendwa Mungu, nisaidie kukupenda kwa moyo wote ili niweze kuwapenda wengine bila masharti.
Kwa jina la Yesu. Amina.



MEJA COLLEEN HUKE
ENEO LA KUSINI MWA AFRIKA

Meja Colleen Huke na mumewe Darren ni viongozi wa Sehemu ya Cape Mashariki katika Teritori ya Afrika Kusini. Wanao watoto wawili wa kiume, Samweli na Danieli. Colleen amefurahia kuhudumu kama afisa katika vikao vya vijijini na jiji, vile vile katika Idara ya elimu na mafunzo katika Teritori hiyo. Shauku yake ni Yesu na huduma ya upatanisho ambao Mungu amempa kila muumini.

# KUSIMAMA KWA AJILI YA WENGINE

AMOSI 5:24

CLEFA JOHN PARMAR

'Lakini hukumu na itelemke kama maji, na haki kama maji makuu' (Amosi 5:24*)*

Sakina alikuwa msichana mzuri. Daima alitaka kupata elimu nzuri na kuwa mhasibu aliyetambulika. Alikuwa mwanafunzi wa kuelewa haraka na alikuwa amejaa ari na shauku. Alikuwa mkarimu na mwenye utu.

Lakini tangu umri mdogo sana alikabiliwa na ukweli mchungu. Akiwa na umri wa miaka 14 alilazimishwa kuwa kahaba na jamaa zake. Alilazimishwa kuhudumia wateja 15 hadi 25 kwa siku. Wakati alipokataa kuhudumia mteja, alipigwa na mlinzi wa danguro. Kila siku alisukumwa kwenye minyororo ya Jahannamu.

Nina hakika kwamba baada ya kusoma hii lazima uwe umeshikwa na hasira na mahangaiko. Mtu anawezaje kuwa mkatili sana kwa msichana kama Sakina? Je, alistahili kutendewa unyama na ukatili kama huo? Kwa bahati mbaya mamilioni ya wasichana husafirishwa na kutumika kama watumwa wa ngono duniani kote.

Kama mfanyakazi wa kijamii nilikutana na Sakina na kumshauri, na nilivunjika moyo kusikia hadithi yake. Ilinikwaza sana na maswali mengi yalinijia akilini mwangu – 'kwa nini jambo hili lilifanyika kwake?', 'haki iko wapi kwa msichana huyu?', 'Je, nini Biblia inatuambia tufanye nini?', 'Ninaweza kufanya nini ili kuwalinda wasichana kama hawa?'.

Nilichogundua ni kwamba, Mungu hapendi udhalimu vilevile. Katika Biblia nzima Mungu anazungumzia haki.

Tulisoma katika Mhubiri 4:1, 'Kisha nikarudi na kuona madhalimu yote yanayotendeka – walakini wale walikuwa hawana mfariji.' Mungu huona machozi yetu. Yeye huona machozi ya maskini na wale walio katika utumwa na moyo wake hulia kwa sauti kubwa kwetu. Yeye ni Mungu wa haki na yeye anataka tuonyeshe haki kwa wengine na kuwasaidia watu wanaodhulumiwa na hawana nguvu.


Hebu tuelewe zaidi kuhusu haki na udhalimu:

Haki inahusu kutumia madaraka kwa usahihi kwa kuhakikisha kila mtu yuko salama, anatetewa na kulindwa.

Udhalimu ni wakati mtu anapotumia mamlaka yake vibaya kwa kuwanyang'anya watu wengine mambo mazuri aliyo wapa Mwenyezi Mungu, maisha yao, uhuru na matunda ya upendo na kazi zao.

Mara nyingi, tunapofikiria juu ya kile kilicho cha haki na kisicho cha haki, tunafikiria serikali, polisi, majaji, na kadhalika – watu wanaotoa haki moja kwa moja. Lakini, kwa sababu wewe si jaji au afisa wa polisi, haimaanishi kuwa huna jukumu la haki.

**'MUNGU ANATUITA KUTUMIE MAMLAKA TULIYONAYO KUHAKIKISHA KUWA KILA MTU – HASA WALE WANYONGE AU WASIO BAHATIKA KATIKA JAMII, AMETENDEWA HAKI.'**



**KUJADILI:**

- Madaraka inatumiwa vibaya katika ulimwengukwa namna gani?
- Kama mtoto wa Mungu utasimama na kuunga mkono vipi wale wanaodhulumiwa?
- Kwa nini unafikiri Mungu anachagua kututumia kama mabalozi wake?

Haki inahusu kutumia madaraka. Mungu anatuita kutumie madaraka tuliyonayo kuhakikisha kuwa kila mtu – hasa wale wanyonge au wasio bahatika katika jamii –wametendewa haki. Kutoka 23:2 inazungumzia suala la haki kwa kutuhimiza kusimama kwa niaba ya wengine, hasa kwa watu wasio bahatika katika jamii au wamenyanganywa madaraka yao.

Isaya 58: 6-7 inaonyesha kwa nini wakati mwingine Mungu hukosa kujibu watu hata wakifunga na kuomba? Nabii Isaya anaangazia katika kifungu hiki kile Mungu anataka kutoka kwa watu wake. Haihusu vyakula mtu anaweza kula lakini badala hatua inayochukuliwa kwa niaba ya na kuhusiana na waliotengwa. mlango huu unaonyesha uhusiano kati ya ibada ya Mungu na matendo ya haki kwa niaba ya wasio bahatika katika jamii. Taifa la Israeli linapewa changamoto ya kuona kuwa uhusiano wao na wengine, hasa wale wametupwa waliotengwa katika jamii, huathiri uhusiano wao na Mungu.



Mpendwa Bwana, nisaidie kuelewa haki ya kijamii ni nini na jinsi ninavyoweza kuleta mabadiliko wakati wa kutenda na kuunga mkono haki. Mola wangu! Nipe moyo wa unyenyekevu ili nisimame kwa niaba ya watu wanaohitaji neema yako. Bwana, nawaombea wasichana kama Sakina ambao wanapitia maumivu ya moyo kila siku.

## CLEFA JOHN PARMAR

TERITORI YA INDIA MAGHARIBI

Clefa anaishi Mumbai na anafanya kazi na shirika lisilo la kiserikali la kupambana na biashara haramu ya kusafirisha binadamu, Misheni ya Haki ya Kimataifa. Yeye ni mfanyakazi wa kijamii na anafanya kazi na waathirika wa ngono, na hutafuta haki kwa wale wanaohitaji ulinzi na utunzaji.



# NJOO UONE

YOHANA 4:1-38

TERRI NEVILLE

Usomaji wetu wa maandiko umefungamanishwa na kwa vichwa viwili. Unapoyawekwa pamoja yanasoma 'Yesu Anasema na Msamaria Mwanamke' na 'Wasamaria Wengi Wanaamini'. Kabla hatujasoma mstari, tunajua kwamba hii haikuwa siku ya kawaida kisimani. Wakati huo huo, wanafunzi hawakulielewa kwa kweli na kwa mfano. Akiwa amechoka kutoka safarini, Yesu alipumzika pale kwa kisima cha Yakobo na wanafunzi wakasafiri kwenda mji wa Sychar kununua chakula. Basi walipo rudi, wanafunzi 'walishtushwa' kumpata Yesu akinena na mwanamke. Ajabu ni kwamba, hakuna mwanafunzi hata mmoja aliuliza' unataka nini?' au 'Kwa nini unazungumza naye?' Hata hivo, mwanamke huyo aliondoka, na kuacha chombo chake cha maji nyuma, na kile wanafunzi walisema ilikuwa, 'Rabi, kula kitu'. Yesu alijibu, 'Nina chakula, chakula kile ambacho hamjui chochote kukihusu'.

Kama ilivyo desturi yake, Yesu mara nyingi alitumia vitu vya ulimwengu vinavyoonekana ili kufafanua ukweli usioonekana waMungu na ufalme wa Mungu. Wanafunzi walichanganyikiwa kama ilivyokuwa desturi yao. Walishangaa, 'Je, mtu alimletea chakula cha mchana? Kutoelewa kwa wanafunzi kunafungua mwanya kwake Yesu kufundisha jambo hili muhimu:

**'YESU ALITUMWA KATIKA MISHENI, YA KIROHO KUWEZESHWA KWA UTUME NA KUENDELEZWA NA THAWABU ZA MILELE ZA KUFANYA MISHENI.'**


'"Chakula changu," alisema Yesu, "ni kufanya mapenzi ya yule aliyenituma na kumaliza kazi yake. Hamsemi, "Miezi minne zaidi kisha mavuno?" Ninakuambia, fungua macho yako na utazame mashamba! Yameiva kwa mavuno ' (Yohana 4:35).

Yesu alitumwa misheni, akiwezeshwa kiroho kwa ajili ya misheni na kuidhinishwa na thawabu ya milele ya kufanya kazi. Maswali hayo hayo wanafunzi hawakuuliza katika mstari wa 27 ina tuongoza kwenye kiini cha utume wa Yesu.

Swali: Unataka nini?
Mwanamke: Hakuna kitu duniani kinachoridhisha kiu cha moyo wangu.
Swali: Kwa nini unazungumza naye?
Yesu: Mimi ndimi Masihi, na baba yangu alinituma kuwapa upendo wa Mungu wenye kutibuka, kufurika, na wa milele. (Yohana 4:13, 26)

‘Fungua macho!' Wanafunzi walimpita mwanamke Msamaria barabarani kuelekea Sychar, wakafanya ununuzi katika viwanja vya mji wa Samaria, na kwa yote, walichokilete ni chakula cha mchana! Wanafunzi walihitajika kukumbushwa juu ya wito yao. Waliitwa kuwa wavuvi wa watu nao walishughulikia mikate kuliko wokovu. Ni wito wa mbinguni kwamba tuamke na kamwe tusiruhusu shughuli nyingi ya kawaida kututoa kwa wito wetu.

Wakati huo huo, mwanamke msamaria aliyetengwa, mwenye maadili potovu akakutana uso kwa uso na Mwokozi wake na maisha yake ikabadilishwa kabisa. Aliyetengwa kijamii akakimbia kwa jamii na kuwaalika wote “njooni muone mtu aliyeniambia kila kitu nilichowahi fanya. Sasa, hii si kama Yesu kujitambulisha kama



**KUJADILI:**

- Ni kwa njia gani wewe au familia yako ya kanisa mmeweka vikwazo kwa ushirika wa binadamu? Na wewe je hunufaika na vizuizi hivyo? Unasumbuliwa?
- Je, maisha yako ni wazi kukutana na wasio amini? Ni hatua gani unaweza kuchukua nje ya eneo lako la kujistarehesha?
- Ni nani unayemdhania kuwa hana matumaini ya kuweza kupokea maisha mapya, ya ukamilifu na uhuru katika Yesu Kristo? Muombe Mungu afungue tena mlango wa mawasiliano.

Masihi kwa mwanamke msamaria aliyedharauliwa na kukataliwa, na ambaye hakuwa na rafiki? Kurejesha sauti yake, hadhi yake katika jamii, na kumbadilishwa kutoka kwa maadili yasiyo kubalika na kuwa kiongozi wa kidini huko Sychar, ni kubadilisha maisha yake yote! Je, si ni kama Yesu kumsamehe dhambi zake na kumfanya kuwa mzima? Na Mungu bado hajakamilisha kazi. Labda macho yake yalitazamia ukombozi wa jamii nzima tangu mwanzo. Je, hiyo si ni kama Mungu?!

Chanzo cha haki na ukamilifu kwa Mungu upo katika utii wa mapenzi ya kujitolea na njia za Mungu. Yesu, akiwa Mungu kikamilifu, alikuwa pia mwanadamu kabisa. Kama Mwana wa pekee wa Mungu, alimtegemea Baba yake kabisa kumtuma, kumuongoza, kumpa nguvu na kumpamahitaji ya kimwili, kihisia, kiakili na kushiriki kiroho na ulimwengu. 'Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe... Kwa kuwa yeye aliyetumwa na Mungu huyanena maneno ya Mungu (Yohana 5:30, Yohana 3:34).

Kama wafuasi wa Kristo, tunafanyaje haki duniani? Utambulisho wetu katika Kristo lazima uwe salama. Lazima tuwe wote ndani! Kujitoa Maisha kikamilifu, upendo wetu na utambulisho wetu unahitajika kwa Utawala wa Yesu, la sivyo huduma yetu hainamaana kwa Mungu. Kama vile tawi kwenye mzabibu haina kuugua na kuumia ili kutoa matunda, tunapokaa katika Kristo, Mungu atazalishaa matunda yake ndani na kupitia kwetu. Ni pale tu tunaposhiriki wema wa Mungu kwetu wenyewe tunakuwa mwaliko hai wa 'kuonja na kuona kwamba Bwana ni mwema'.

Tunapotoa maisha na wito wetu, tunapojitolea kwa unyenyekevu, Mungu huzidisha ili kukidhi njaa na kiu ya waliopotea na kuwaleta katika Ufalme. Inua macho yako, na uangalie mashamba! Tazama haki itelemke hadi miisho wa dunia, na kamwe usidhoofishe na kudharau nguvu ya mazungumzo ya kiungu.



Wape nguvu na matumaini wanaoonewa na kuwanyenyekesha wadhalimu ili waende wakashuhudie hadithi zao kwa utukufu wa Mungu na mshangao wa watu.


**TERRI NEVILLE**

TERITORI YA MAREKANI KUSINI


Terri anamtumikia Bwana kupitia Jeshi la Wokovu kama Mkurugenzi wa Haki ya Jamii Kituo cha Rasilimali (SJRC) Teritori ya Marekani Kusini. Imenjengwa kwenye Chuo Kikuu cha Trevecca Nazarene, SJRC ni maabara na kichocheo cha kujifunza iliyojitolea kwa kuhamasisha, kujulisha na kutayara wanaongozwa na Roho Mtakatifu, na matendo bora ya utume. Terri pia ni mwanachama aliyeteuliwa wa Baraza la Kimataifa la Maadili na Masuala ya Kijamii na Msaidizi Sagenti Mkuu wa Teritori. Katika wakati wake wa bure pasipo na shughuli, Terri anapenda Barabara pana, muziki, kucheza michezo, na zaidi ya yote, kupata muda na mumewe Rob, mwanawe Ben na bintiye Riley.



# HAKI KATIKA KILA KONA

WAGALATIA 5:13-26
MEJA NI KOMANG ARIANI WIBOWO

Katika ulimwengu wa sasa ubinafsi na kupenda ali hufanya iwe vigumu kutafuta haki. Haki imeadimika na kuwa ghali na inaonekana kana kwamba udhalimu hutokea karibu kila nyanja ya maisha.

Haki ya kijamii ni neno linalotumika kuelezea vitendo na mawazo, yote ya kitaifa na hata ya ulimwengu. Lakini ulimwengu unaweza kuwa na haki katika kila kona yake? Isaya 1:17 inasema: 'Jifunze kutenda mema; kutafuta haki. Kulinda Walio dhulumiwa. Kumtetea yatima; kuomba kwa kesi ya mjane, inamaanisha kuzungumzia haki sawa kwa wanadamu wote. Kwa karne nyingi kumekuwa na masuala ya udhalimu wa kijamii, na mambo mengi yanayohusika yanamaanisha kuwa masuala hayajawahi kutatuliwa, hata leo. Lazima tutambue usawa kama haki kamili kwa kila mwanadamu.

Udhalimu hutokea kwa njia mbalimbali, katika mazingira yote na, hata zaidi ya kutisha, ndani ya familia nyingi na kaya(households). Athari za migogoro husababisha mgawanyiko katika familia, mfarakano katika jamii na kuleta hisia ya dhiki, chuki na wivu; hisia ambazo zinazidi kuwa na nguvu katika kuwadhibiti wale ambao hawaja tendewa haki, wakati mitazamo ya kiburi na ya kiholela ya watu wenye tamaa ambao wanaendelea kutawala. Katika kukabiliana na hali hii, tunapaswa kufanya nini?


Tunakumbushwa na maandishi ya Mtume Paulo katika Wagalatia 5:13-14:

*Enyi kaka zangu na dada zangu, mliitwa kuwa huru. Lakini msitumie uhuru wenu kujiingiza katika mwili; badala yake, kutumikia kila mmoja kwa unyenyekevu katika upendo. Katika sheria nzima imetimizwa katika kutii amri hii moja: "Mpende jirani yako kama wewe mwenyewe".*

Kifungu hiki kinazungumzia uhuru – neno zuri la kusikia. Tunapaswa kufanya nini kama Wakristo kwa Uhuru ambao tumepewa?

Watu ambao wamewekwa huru hawapaswi kutumia uhuru wao kwa kutenda dhambi, bali kuwahudumia wengine kwa upendo. Huu ni ujumbe wazi - kwamba wale ambao wamewekwa huru na kupendwa katika Kristo wanapaswa kuchangia kusaidia kuunda haki na kujali, popote tulipo, kulingana na upendo. Yeremia 22:3 inasema: 'Hiki ndicho Bwana asemacho: Tenda yaliyo ya haki na kweli. Muokoe aliyedhulumiwa kutoka kwa mikono ya mnyang'anyi. Usimkose au kumvuruga mgeni, yatima au mjane, na wala kumwaga damu isiyo na hatia mahali hapa'

**'WALE AMBAO WAMEWEKWA HURU NA KUPENDWA KATIKA KRISTO WANAPASWA KUCHANGIA KUSAIDIA KUJENGA HAKI NA KUJALI.'**



**KUJADILI:**

- Tunawezaje kuangaza haki ya Kristo katika maisha yetu wenyewe, na kwa familia zetu na watu wengine? Vipi kuhusu sisi wenyewe na maisha yetu kama wanawake wa Kikristo. Tunaweza kuangaza haki ya Kristo kwa ajili ya familia zetu na watu wengine?
- Je, tumeshiriki katika mapambano dhidi ya udhalimu yanayotuzunguka?
- Je, unataka kutumiwa na Mungu kuonyesha haki yake na upendo wake?

Acha tujifunze jinsi ya kuhifadhi uhuru wetu katika Kristo na kuleta athari katika mazingira yetu ili kutambua haki katika jamii zetu:

1. Sisi, kama wanawake wa Kikristo, tunatakiwa kibinafsi kudumisha uhuru wetu katika Kristo, kwa kuweka utakatifu wa maisha, iwe katika sala, ibada, shughuli au maneno, ili njia yetu ya zamani ya maisha isijirudie. Wagalatia 5:13 inasema 'Lakini usitumie uhuru wako kujiingiza katika mwili; Bali uutumie katika upendo. Wakati unafanya hivyo, ushuhuda wako na mfano utatenda kama motisha na kuwahimiza wengine kuiga njia yako ya maisha.
2. Kupitia uhuru tulio nao, Mungu atatutumia kufanya kazi zake – kuwatumikia na kuwasaidia majirani zetu ambao bado wanaishi katika dhambi. Tunafanya hivyo kwa njia ambazo hazibagui (moyo kwa Mungu na mkono kwa mwanadamu), lakini kwa upendo na haki kama Mungu anavyofanya katika maisha yetu. Kama Kumbukumbu la Torati 32:4 inatukumbusha 'njia zake zote ni za haki'.
3. Haki ya Mungu ni kamilifu. Uhuru katika Kristo ni sawa, kama nguvu za Mungu tunavyoishi katika maisha yetu ili kutukamilisha kama yeye mwenyewe na kufanya kazi zake.

Kwa hiyo kile kilichoandikwa katika Amosi 5:24 - 'Lakini hukumu na itelemke kama maji, na haki kama maji makuu!' - yataendelea kutokea. Wengi watabarikiwa na sisi, kama wanawake ambao wamewekwa huru katika Kristo, watahusika katika kuunda na kutafuta haki.

Sasa hebu tuchukue muda, kama wanawake wa Kikristo ambao kwa muda mrefu hushiriki katika kazi ya Mungu, kuonyesha haki kwa kila mmoja.

Natumaini maswali ya majadiliano yanaweza kutusaidia kuwa watu wa ajabu mbele za Mungu na kwa wengine. Anza kwa kuzingatia haki ya kijamii kwa ajili yenu wenyewe na familia zenu. Kumbuka, pamoja na Mungu tunaweza!

Baba Mungu, asante kwa kutuweka huru kama uumbaji wako maalum. Tusaidie kuwa sisi kuwa chombo cha amani katika ulimwengu huu, ili watu wanaotuzunguka wataona upendo wako na kuwa na tumaini ndani yako. Amina.


**MEJA NI KOMANG ARIANI WIBOWO**

TERITORI YA INDONESIA


Meja Ni Komang Ariani ni Afisa wa Miradi ya Huduma za Jamii na Mawasiliano ya Taifa Mshirikishi anayepambana na Biashara Haramu ya Binadamu nchini Indonesia. Kama mfuasi wa Yesu Kristo, anatamani kuwasiliana/kuwasilisha upendo wa Mungu kwa kila mtu kwa njia ya maneno na matendo.



# JE, UTAYATOA MAISHA YAKO?

MEJA EDITH LOUZOLO

1 YOHANA 3:11-24

**'Kwa maana huu ndio ujumbe uliosikia tangu mwanzo: Tunapaswa kupendana... Hivi ndivyo tunavyojua upendo ni nini: Yesu Kristo aliyatoa maisha yake kwa ajili yetu. Na tunapaswa kuweka maisha yetu kwa ajili ya ndugu zetu na dada zetu. Ikiwa mtu yeyote ana mali na anamwona ndugu au dada mwenye mahitaji lakini hana huruma juu yao, upendo wa Mungu unawezaje kuwa ndani ya mtu huyo? Wanangu wapendwa, tusipende kwa maneno au hotuba bali kwa matendo na kwa kweli' (1 Yohana 3:11, 16-18).**


Ulimwengu huu unaweza kuwa sio wa haki kwa njia ambayo watu wanatendewa, na kuna ukosefu mkubwa wa usawa. Kama Wakristo, tunapomwona ndugu au dada mwenye mahitaji, kama 1 Yohana 3:17 inavyosema, lazima tuwaonyeshe huruma. Tukipuuza kufanya hivyo, lazima tujiulize swali 'Upendo wa Mungu unawezaje kukaa ndani mwetu?' Tunaishi katika ulimwengu ambapo lazima tulilie haki ya kijamii.

Motisha katika kilio chetu cha haki ya kijamii imeangaziwa katika Mithali 31: 8-9, kama Biblia inavyosomeka: 'Sema kwa wale ambao hawawezi kujizungumzia wenyewe, kwa ajili ya haki za wote ambao ni wenye dhambi. Ongea na uamuzi kwa haki; kulinda Haki za maskini na wenye mahitaji.

Biblia inatufundisha kwamba Mungu ni Mungu wa haki. Njia zake zote ni za haki. Wazo la Biblia la haki ya kijamii linahusisha kuwajali na kuwatunza maskini na walioteswa. Biblia mara nyingi inazungumzia yatima, mjane na mgeni - yaani watu ambao hawakuweza kujilisha wenyewe au hawakuwa na mfumo wa msaada. Taifa la Israeli liliamriwa na Mungu kutunza jamii isiyo na bahati, na hatimaye kushindwa kwake kufanya hivyo kwa kiasi fulani ya hukumu yake na kufukuzwa kutoka nchi hiyo. Kama sehemu ya maono ya Biblia ya haki, Tunafundishwa kwamba Mungu anatuona sisi sote kama viumbe vya thamani sawa: Mungu aliumba wanadamu kwa mfano wake (Mwanzo 1:27), kila mtu ametenda dhambi na ametengwa kutoka kwa Mungu (Warumi 3:23) na chini ya damu ya Kristo mgawanyiko wa mwanadamu hauna maana na waumini wanakuwa familia moja ndani yake (Wagalatia 3: 27-29).

Haki katika Biblia inamaanisha haki kwa wote. Upendo unapaswa kuonyeshwa kwa wote, bila kujali historia: 'Na wakati anakaa pamoja nanyi katika nchi yenu, hamtamdhulumu. Mgeni ambaye anakaa nanyi atakuwa kama mzaliwa miongoni mwenu, nanyi mtampenda kama nafsi yanu, kwa sababu mlikuwa wageni katika nchi ya Misri; Mimi ni Yahweh Mungu wenu (Mambo ya Walawi 19: 33-34). Sheria hizi katika Mambo ya Walawi 19 zilikusudiwa hasa kuwalinda wakimbizi na wahamiaji kwa Israeli. Hivyo, haikuwa tu Waisraeli ambao walilindwa na mfumo wa Mungu wa haki (Sheria), watu wa nje pia walipata ulinzi.

## 'KAMA WAKRISTO, TUNAPOMWONA NDUGU AU DADA MWENYE MAHITAJI... LAZIMA TUWAONYESHE HURUMA.'



**KUJADILI:**

- Unawezaje kuzungumza kwa wale ambao hawawezi kuzungumza wenyewe?
- Uko tayari kujitolea nini kwa ajili ya haki kurejeshwa?
- Ni hatua gani uko tayari kuchukua haki kukuzunguka?

Hata hivyo, haitoshi tu kulia kwa haki ya kijamii. Lazima pia tuchukue hatua, kama vile Yesu alivyofanya. Maandiko ya, 1 Yohana 3:11-24, yanasisitiza nguvu ya upendo tunapoishi nje ya imani yetu. Katikati ya mistari iliyochaguliwa ni 1 Yohana 3:16: 'Hivi ndivyo tunavyojua upendo ni nini: Yesu Kristo aliyatoa maisha yake kwa ajili yetu. Na sisi inatupasa kuweka maisha yetu kwa ajili ya ndugu na dada zetu. Fungu hili linatuambia mambo mawili: Yesu aliweka chini maisha yake kutokana na upendo wake kwetu, na tunapaswa kujitahidi kuwapenda wengine kama Yesu anavyotupenda. Tunapotazama mistari mingine sawa katika Yohana 15:13, tunasoma kwamba 'upendo mkubwa hauna mtu kuliko huu, kuweka maisha ya mtu kama rafiki wa mtumwingine.' Mafungu haya yanatutayarisha kuishi na kutenda kwa kiasi kikubwa katika jina la upendo, kama vile Yesu alivyofanya.

Katika Agano la Kale, tunapata mfano wa mtu ambaye yuko tayari kufa kwa jina la upendo katika Esta: 'Kisha Esta alituma jibu hili kwa Mordekai:"Nenda, uwakusanye Pamoja Wayahudi wote walioko Susa, na ufunge. usikule au kunywa kwa siku tatu, usiku au mchana. Mimi na wahudumu wangu watafunga kama uvyofanya. Wakati hili likifanyika, nitaenda kwa mfalme, ingawa ni kinyume cha sheria. Na kama nikiangamia, ninaangamia"' (Esta 4:15-16).

Kwa kusema 'Nikiangamia, naangamia', Esta anatambua kwamba, ingawa kujua hatari yake ni kubwa na dhahiri, na kujua kutokuwa na uhakika wa akili ya mfalme na ukali aliouonyesha kwa Vashti, kamwe asingeweza kamwe kupuuza wajibu wake kwa Mungu na watu wa Mungu. Anaamua kwenda kwa mfalme, na kujitupa juu ya Mungu, akiomba usalama na mafanikio. Anaashiria kwamba kwa haraka na kwa furaha atahatarisha maisha yake kwa manufaa ya watu wake na kumheshimu Mungu. Esta anaamini kwamba kama kupoteza maisha yake kulikuwa ni furaha ya Mungu, basi anapaswa kuipoteza. Yeye aliridhika katika mapenzi yake kwa maisha yake na akajiacha mikononi mwake kabisa.

Mistari ya kufunga ya dhabihu yetu ya Maandiko iliyochaguliwa ya Esta: 'Tuna imani mbele za Mungu na kupokea kutoka kwake chochote tunachoomba, kwa sababu tunatii amri zake na kufanya kile kinachompendeza. Yule ambaye huzishika amri za Mungu ndani yake, na yeye ndani yao. Na hivi ndivyo tunavyojua kwamba anaishi ndani yetu: Tunajua kwa Roho alitupa' (1 Yohana 3:21-22, 24). Yesu anatuita tutafute na kutenda haki kila mahali, kama vile Esta alihatarisha maisha yake kwa ajili ya watu wake, na kama Yesu mwenyewe alivyoyatoa maisha yake kwa ajili ya watu wa Mungu aliowapenda.



Bwana, washa/chochea moto wa upendo wako ndani yangu ili niweze daima kuwapenda wengine kama wewe. Amina.

## MEJA EDITH LOUZOLO

### KOMAND YA RWANDA NA BURUNDI



Meja Edith Louzolo ameolewa ni mama wa watoto wanne. Amekuwa Afisa wa jeshi La Wokovu kwa miaka 28. Amewahi kuwa afisa katika vikao mbalimbali katika Teritori ya Kongo (Brazzaville) na pia Teritori ya Ubelgiji, katika kazi za kijamii na katika Chuo cha Mafunzo cha Maafisa. Kwa sasa anahudumu kama Katibu wa vyama vya Wanawake katika Komand ya Rwanda na Burundi.

# KUSIMAMIA HAKI

ZAKARIA 7

MEJA JASHIBEN D. KHRISTI

**Hiki ndicho Bwana Mwenyezi alisema: 'Toa haki ya kweli; onyesha rehema na huruma kwa kila mmoja. (Zakaria 7:9).**

Bado nakumbuka darasa langu la uchumi ambalo profesa wetu alirejelea baadhi ya vyumba vya kifahari na vidogo, vibanda ambavyo vilijengwa bega kwa bega. Wakati familia moja inafurahia zaidi ya wanavyohitaji, nyingine ni kuhangaika kula, kupata maji safi ya kunywa, vituo vya afya na bidhaa za usafi, na maisha katika mazingira yasiyo salama.

Miaka imepita lakini hali hii ya ulimwengu bado ni sawa. Inaonyesha picha wazi ya udhalimu wa kijamii, Ambapo hali ya watu masikini inapuuzwa.

Kwa ujumla, Haki ya kijamii inamaanisha watu wote wanapaswa kuwa na upatikanaji sawa wa utajiri, afya, ustawi, haki na fursa. Haki sio ya hiari, ni muhimu; sio kitendo cha wakati mmoja bali ni kitendo endelevu mchakato. (*continuous process*) Tukiiangalia Biblia, haki ya kijamii imefupishwa katika amri moja - 'Mpende Jirani yako kama wewe mwenyewe'. Upendo haufanyi chochote kibaya kwa jirani yako; badala yake, uko tayari kuweka maisha yako kwa ajili yao.

Mungu wetu anaonyesha upendo wake na huruma bila kuchoka. Mtunga Zaburi anasema, 'Hatutendei kama dhambi zetu tunastahili au kutulipa kulingana na maovu yetu' (Zaburi 103:10). Ingawa Waisraeli walikuwa wamepata uzoefu wa miujiza mingi iliyofanywa na Mungu, walikuwa na shukrani kwa ajili ya usalama, chakula, maji, n.k. Hata hivyo Mungu alionyesha upendo na huruma.


Tunasoma katika Biblia kuhusu upendo wa mara kwa mara wa Bwana wetu Yesu Kristo kuelekea dhiki na mahitaji wakati wa huduma yake duniani. Alipoona umati wa watu, alikuwa na huruma Juu yao, kwa sababu walinyanyaswa, na wasiojiweza, kama kondoo bila mchungaji' (Mathayo 9:36). Yesu Kristo ameweka mfano wa haki ya kweli, upendo na huruma kwa wengine.

**'UPENDO HAUFANYI KITU CHOCHOTE KIBAYA KWA JIRANI YAKE; BADALA YAKE, UKO TAYARI KUTOA MAISHA YAKO KWA AJILI YAO.'**

Sura ya saba ya Zakaria inahusika na maombolezo na kufunga kama mazoezi ambayo watu walikuwa wakifuatilia kwa Miaka 70. Hata hivyo, Mungu hakuwa na furaha na maombolezo yao na kufunga kwani walikuwa wakienda kinyume na amri ya Mungu mistari ya 5-6. Kwa hiyo, Mungu alinena nao kupitia Zakaria, akiweka wazi kile anachotarajia kutoka kwa watu wake: kutenda dhidi ya suala la udhalimu wa kijamii.

Tunapata hali kama hiyo leo. Watu huwa wanafuata mazoea ya kawaida ya sakramenti na sherehe za kidini kwa upofu. Ukosefu wao wa upendo na huruma husababisha wao kushindwa kuona kwamba wana jukumu muhimu katika ukiukaji wa haki za msingi ya watu ambao ni waathirika wa ubaguzi na udhalimu.

Machoni pa Mungu, watu ni muhimu zaidi kuliko mazoea. Yeye haangalii misimamo, utu au ustawi wa mtu, wakati wanadamu wanajihusisha sana na haya yote mambo. Mungu anatutarajia tusipuuze hisani bali kuhudumu



**KUJADILI:**

- Ni dhuluma gani umegundua hutokea karibu na wewe?
- Je, mwitikio wako dhidi ya dhulma hizi ulikuwa nini?
- Unawezaje kuitikia wito wa Mungu juu ya maisha yako kushiriki katika misheni yake?

kwa upendo bila ubaguzi. Masuala mengi yanayohusiana na haki za kijamii yanajitokeza kutokana na uchoyo, ubinafsi na njaa ya kuawala au nafasi. Kama watu wanaelewa hili, hakutakuwa na umaskini wala biashara ya wanadamu; hakuna vita au wakimbizi; Wanaume hawana upendeleo dhidi ya wanawake. Na lau kama wangelifanya walio waitikia, na nchi, na watu wangepata fursa sawa katika kila sekta. Kutokana na ukosefu wa huduma za afya au fedha za kutotosha watu hufariki, na wanawake na watoto wanasafirishwa katika nchi nyingi. Hali hizi zinaonekana wazi, lakini watu wanafunga macho yao, kugeuza nyuso zao na kutembea kama kuhani na Walawi ambao walibadilisha njia yao baada ya kumwona mtu amelala nusu amekufa kando ya barabara huko Yeriko. Hata hivyo, Msamaria mwema alionyesha huruma kwa mtu huyo na kuokoa maisha yake. Masuala ya haki za kijamii yanaweza kutokea kuhusiana na kivitendo. Kipengele chochote cha jamii ambacho kutokuwepo kwa usawa kinaweza kutokea kutokana na ubaguzi usio wa haki au sera.

Hali hii itabadilika lini? Nani ataibadilisha? Lazima tujitokeze kubadilisha hali hii. Ni wakati wa kutenda. Juhudi za ajabu zinafanywa na Umoja wa Mataifa, serikali na mashirika mengine. Wanafanya bora kwa kuunda sheria mpya na kuchochea kampeni za uhamasishaji. Tunaweza kufahamu masharti hayo, lakini tunahitaji kubadilisha mawazo yetu ili kuleta mabadiliko katika jamii yetu, nchi yetu. Hebu tuwe na mawazo kama ya Kristo, ambaye alikuwa amejaa haki, upendo na huruma. Sisi ni wafuasi wake; tunahitaji kufuata nyayo zake. Hebu sikiliza kile Mungu anasema, 'Toa haki ya kweli; Onyesha rehema na huruma kwa kila mmoja (mstari wa 9).

Jenerali Brian Peddle ametupa wito wa kuchukua hatua; haijalishi sisi ni nani au tunahudumu wapi, bila kujali miadi au msimamo, lazima tuitikie wito na kufanya kama Mungu anavyotuamuru.



Mpendwa Bwana, nisaidie kutoa haki kwa wanyonge na wasio na baba; kudumisha haki ya walio waliodhulumiwa na kuteswa. Nipe moyo wenye huruma kutimiza wito wangu wa kuhumu. Amina.


**MEJA JASHIBEN D. KHRISTI**

OFISI YA KITAIFA YA INDIA

Meja Khristi ni afisa wa Teritori ya India Magharibi, akihudumu katika Ulinzi wa Watoto Mtaalamu wa India, anayeishi Ofisi ya Taifa ya India mjini Kolkata. Amehudumu kama afisa kwa miaka 28 na ana shahada ya uzamili(*Masters*) katika Kazi za Jamii




# MOYO WA HAKI

MARKO 10:35-45

KAPTENI MARIE LANGE DRUART

Hivi karibuni nilikuwa nikitazama makala kuhusu suala la 'ndoa ya muda' nchini Iran, *Nikah mut'ah*, pia inayojulikana kama Sigheh, kwa kweli maana ya 'ndoa ya kujifurahisha'. Katika aina ya ndoa hii, mwanaume anaweza kuwa na wake wengi wa muda jinsi anavyotaka, na wake wanne wa kudumu, na ana haki ya kuvunja mkataba alioweka wakati wowote anaohitaji. Wairani wengi wa kidunia wanadanganywa na kile wanachokiona kuwa unafiki wa wahubiri ambao walifanya matumizi makubwa ya ndoa ya muda kwa miaka mingi lakini inapingana na kuoa kabla ya ndoa au ndoa za nje ya ndoa kimapenzi. Mazoezi ya Sigheh yawawezesha wanaume wengi walioolewa kuingia katika ndoa za muda na wanawake zaidi ya wake zao na pia inaruhusu kuanzishwa kwa nyumba za usafi wa kimwili.

Tunawezaje kubaki bila kutikishwa na matendo hayo ya kutisha kwa wasichana na wanawake wadogo katika ulimwengu wetu? Tunawezaje kugeuza uso wetu kutoka kwa unafiki kama huo? Swali bora la kuuliza ni, kama mfuasi wa Kristo, ni nini wajibu wetu kuelekea kwenye unyanyasaji kwa wengine na ni vipi tunathubutu kuchukua hatua?


Kupitia kifungu hiki cha Marko 10:35-45, tunajifunza kwamba kila mfuasi wa Kristo anaweza kupitia mateso, lakini wameitwa kutumikia watu licha ya mapambano ya kibinafsi. Tofauti na Yakobo na Yohana, wote wakiwa na nia ya kuwa upande wa utukufu wa Yesu, kila mwanafunzi lazima ajue kwamba njia ya kuwa upande wa Yesu si kwa kudai kuinuliwa katika hali. Njia ya kuwa upande wa Yesu ni kuwa tayari kunyenyekea, kuwa mtumishi wa wote. Kumbuka muktadha ambao watu hao wawili kwa ujasiri walimwuliza Yesu kuhusu nafasi yao ya baadaye: Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake jinsi atapitia mateso na aibu kabla ya utukufu. Ni jambo la kushangaza sana kwani badala yao kuwa makini na kile Yesu aliwaambia, lengo lao bado ni juu yao Wenyewe!

Kile wanafunzi walishindwa kuona ni kwamba Yesu aliwafundisha kuhusu masharti yanayohitajika kufikia utukufu wake. Alitumia picha mbili: kwanza, 'kikombe', picha ya yaliyomo au hali ambazo ni ngumu na pili, 'ubatizo', kwa kweli maana yake 'kutumbukizwa', hapa kufikisha kifo cha Yesu na baadaye Ufufuo. Yesu alijua kwamba kabla ya kuingia katika utukufu wa Baba yake, atalazimika kunywa kutoka kikombe cha mateso hadi hatua ya kifo. Wanafunzi hawakuelewa maana ya ombi lao.

**'HAIJALISHI MATESO YETU SASA, INATUPASA TUJITAHIDI KUWA UPANDE WA YESU' KUTUMIKIA UBINADAMU KWA UNYENYEKEVU.'**

Sasa, ikiwa tutaangalia katika kifungu hiki kutoka kwa mtazamo wa kijamii kwa ajili ya haki, tunaweza kukiri kwamba kila mtu anakabiliwa na udhalimu wa kitabia au kutochukuliana kwa haki wakati mwingine, ni hali ya mateso. Kama vile Yesu alijua kwamba Yakobo na Yohana watashiriki kikombe cha mateso kwa njia yao wenyewe sisi, kama wanafunzi wa Kristo, twatambua kwamba tutapitia kwa shida katika maisha haya kwa sababu mbalimbali. Hata hivyo, kile tunachojifunza kupitia uzoefu kinatuwezesha kuangalia zaidi ya maumivu yetu wenyewe kwa utaratibu kuzingatia jinsi ya kupambana kwa niaba ya mtu mwingine na kutukuza mwokozi wetu.

Kidogo zaidi katika majadiliano, Yesu aliwakumbusha wanafunzi kinachofahamika kwa kutumika katika ufalme wa Mungu. Anaonyesha utukufu dhidi ya unyenyekevu unapotofautishana. 'watawala' au maafisa wakuu wanaotumia mamlaka juu yao na 'mkuu' katika Ufalme wa Mungu ambao ni watumishi wa wote. Isitoshe, wafuasi wa Kristo lazima wawe na lengo la kusaidia kila mmoja anayepitia mambo yasio ya haki, akiwahudumia kwa unyenyekevu na moyo wa mtumishi. Katika Marko 10:43 Yesu aliwaambia, 'Yeyote atakaekuwa mkubwa kati yenu lazima awe mtumishi, kumbuka jinsi neno, mtumwa, anatumiwa katika kifungu 44 ambacho kinasisitiza mkao muhimu wa utii kwamba neno 'mtumishi' linafanya sivyo, ili kuweza kusimamisha maana kamili ya utumishi katika Ufalme wa Mungu. Neno 'mtumwa' lasisitiza



**KUJADILI:**

- Fikiria wakati wowote ambao umehudumu kwa ajili ya utukufu wa mwanadamu na sio utukufu wa Kristo.
- Nani unaweza kuunga mkono ndani ya jiji lako kwa sala, wakati au fedha?
- Kujua moyo wa Yesu kwa kuhudumu katikati ya shida, ni hatua gani za vitendo unazoweza kuchukua kuwa sauti kwa wasio na sauti licha ya mapambano yako binafsi?

mtumishi kwa yule anayehudumiwa. Hii inatukumbusha jinsi tulivyo fungwa kuwa chini ya Yesu tukiwatumikia wenzetu.

Lengo la mfuasi wa Kristo linapaswa kuwa kuwathamini wengine zaidi ya nafsi yake. Kama 'Mwana wa Adamu hakuja ili ahudumiwe, lakini kuhudumu, na kutoa maisha yake kama fidia kwa wengi'', wanafunzi wote wanahimizwa kufuata kanuni hii. Kuwa na moyo wa haki kupitia huduma ni pamoja na kumwaga kwa wale ambao huenda hawakuwa na fursa katika suala la utajiri, nyenzo, elimu, hali ya kijamii au jinsia.

Katika matumizi ya Neno, kujua kuhusu tabia hii ya 'ndoa isio ya kudumu' au udhalimu mwingine wowote wa kijamii kwamba tumefanywa kujua haipaswi tu kutuchochea kuhamishwa kihisia, lakini pia inapaswa kutusababua kuelekea Kitendo. Mambo mengi yanaweza kufanywa ili kutoa sauti kwa wanawake na wasichana hao. Kuongeza uelewano kuhusu hali hiyo inaweza kuwa hatua ya kwanza. Hatupaswi kuwa wataalam wa kuanza mchakato, lakini tunaweza kukutana nao na kujifunza kutoka kwa wataalamu na kushiriki kwa njia fulani. Kama ulimwengu wetu umejawa na udhalimu wa kijamii, bila kujali mateso ya kibinafsi ya sasa, tunapaswa kujitahidi kuwa upande wa Yesu, tukitumikia binadamu kwa unyenyekevu.

Bwana, asante kwa kuwa mfano wa kweli wa kuwahudumia binadamu kwa njia ya mateso. Tafadhali tusamehe sisi tunapotumika kutafuta kukiri badala ya unyenyekevu. Tusaidie kuhudumu na hamu kubwa ya kuleta haki katika mzunguko wetu wa ushawishi, kukataza kwamba mateso yetu wenyewe kutufanya tujikite ndani na kupuuza ulimwengu wa udhalimu ambao unapigania kuwa sahihi. Amina.

## KAPTENI MARIE LANGE DRUART

TERITORI YA UFARANSA NA UBELGIJI



Kapteni Marie Lange Druart anahudumu kama afisa wa kikao huko Liège, Ubelgiji, lakini ni mzaliwa wa Ufaransa. Ameolewa na ana watoto wawili. Marie ana moyo wa kuinua uhamasishaji kuhusu utumwa wa kisasa na anafurahia kufanya uhusiano mpya na watu tofauti tofauti popote Bwana anamuelekeza.

# NINI MUNGU ANAULIZA KUKUHUSU WEWE?

MATHAYO 25:31-46
MEJA VALESKA JARA

**“Mfalme atajibu: Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndungu zangu walio wadogo mlinitendea mimi”. (Mathayo 25:40).**

Jinsi gani sisi twaweza kufanya haki kwa kuwa mfuasi wa Kristo? Kwa kusoma swali hili, inaonekana kwamba jibu dhahiri linakuja katika njia ya wazi, kwa kuwa Wakristo mara nyingi hufanana na viumbe wenye haki. Hata hivyo, kufanya haki ni kama tofauti, karibu jukumu la kipekee, tunapopambana na muda mrefu kukuwa wema. Kufanya haki ni jambo lisilo waziwazi kwa kila mtu. Tunakuja kulifikiria kama wito maalum au tofauti, kwa baadhi tu.


Ukweli ni kwamba tangu Agano la Kale wito wa kufanya haki ni kwa kila mtu, kwa kuwa tunaishi katika ulimwengu ambapo, kwa sababu ya dhambi, udhalimu hutawala.

Wito wa kutenda haki unaweza kupatikana katika Mika 6:7-8: 'Je, Bwana atafurahishwa na maelfu ya kondoo waume, au kwa Mito elfu kumi ya mafuta? Je, nitamtoa mzaliwa wangu wa kwanza kwa kosa langu, matunda ya mwili wangu kwa ajili ya dhambi zangu? Wewe umeambiwa kile Bwana anatarajia kutoka kwako: kufanya haki, kwa kupenda rehema, na kujinyenyekeza mwenyewe mbele ya Mungu. Katika kifungu hiki, tunaweza ona wazi kwamba haki ambayo Mungu anatarajia kutoka kwa watu wake ni vitendo. Ilikuwa wakati njia ya ukombozi ilikuwa kupitia sadaka na madhabahu. Kufanya haki sio tu kwa amri bali kwa upendo, ni kile ambacho Mungu aliwahitaji wajifunze kufanya. Bila shaka watu walikuwa wakifanya ibada ya sadaka, Lakini kwa macho ya Mungu ilikuwa ni bure ikiwa walikuwa na dhuluma kwa ndungu.

Hata hivyo, kutenda uadilifu sio chaguo ambalo wengine wanaweza kufanya tu, lakini ni sehemu muhimu ya kuwa mfuasi wa Kristo. Sehemu hii ni ya muhimu ya kuonyesha wakati tukiwa na mabadiliko yetu wenyewe na Mungu. Tunapokuja miguuni pa Yesu Kristo bila sababu au madhumuni yeye hujaza maisha yetu na furaha, matumaini, na upendo, maandiko yanasema kwamba upendo wa Mungu imemwagwa mioyoni, upendo wa Mungu ni injini inayo tufanya tusiangalie kwa tatizo letu ama hali na inatufanya sisi kuangalia maisha ya wengine, kujiweka katika nafasi ya hao wanao teseka. Wakati haya hutokea sisi kwa dhati hutaka kufanya yale tunaweza kwa kupuuza mateso yao kwa vyovyote vile.

1 Yohana 3:18 inasema, Wanangu wapendwa, tusipende neno wala kwa ulimi, bali kwa tendo na ukweli. Njia ya kuufanya ulimwengu uone kwamba sisi ni wafuasi wa kweli wa Kristo ni kwa kuonyesha upendo wake, sio kwa midomo, na sio kwa upendo unaokaa kwenye madhabao, bali upendo wa kivitendo unaoshuka kwa ulimwengu unaouhitaji.

**'UPENDO WA MUNGU NI INJINI INAYOTUONGOZA KUKOMESHA KUANGALIA TU KWA SHIDA ZETU, AMA HALI NA INATUELEKEZA KUANGALIA MAISHA YA WENGINE.’**



**KUJADILI:**

- Jinsi gani Unaweza kuitikia wito wa kufanya haki katika jamii yako?
- Ni zipi baadhi ya vikwazo ambavyo wafuasi wa Kristo wanakutana nayo katika njia ya kufanya haki?
- Faraja ya Wakristo waliohifadhiwa leo katika makanisa yetu inawazuiaje kumwona Kristo akiteseka katika kutokuwepo kwa usawa wa kijamii wa leo?

Upendo ni kuonyesha kupitia hatua ya wazi kwa majirani zetu. Sisi lazima tuonyeshe upendo unaoonekana kwa macho yenye nia ya mahitaji ya watu karibu nasi, upendo unaokumbatia, shiriki, upendo unaowaendeleza wengine, unaofundisha, wenye kujenga, unaoonekana huru katika jamii tupoishi, wenye unatambua wahitaji na kukidhi mahitaji yao. Sisi Lazima tuonyeshe upendo wa Kristo mwenyewe kitembea katikati ya haja na kuwafikia, kupitia kwetu, kwa hilo hitaji.

Mungu anataka kuheshimiwa na watu wake, sio tu na wakubwa na mipango iliyo andaliwa, lakini tunapopenda kila mmoja na hasa tunapoongeza upendo huo kwa wale wanaoishi katika hali ngumu ndani ya jamii na zaidi.

Mathayo 25:40 inasema, 'Nawaambia ukweli, lolote mlilomfanyia mmoja wapo wa hao ndugu zangu, mulinitendea mimi'. Kifungu hiki kinatupa sisi nafasi na changamoto ya kufanya haki. Hutoa orodha ya hatua ambazo hutufikia na kwamba tunaweza kufanya hali ya dhulma inayo dhuru majirani wetu. Njaa, kiu, ukosefu wa mavazi ni madhara ya kutokuwepo kwa usawa ambao ulimwengu wetu huzalisha zaidi na zaidi kila siku. Mizani imefungwa kwa mifano ya kiuchumi ambayo inapendelea yule ambaye ana zaidi na kuhatarisha yule aliye na kidogo; mara nyingi tunapata ubaguzi wenye sifa ya mgeni na ukosefu wa huruma na wale walionyimwa uhuru na wachache wengine majibu ya wale walioko kulia na kushoto, Bwana ni lini tulikuona ama ni lini hatukukuona wewe? Tunaishi hivyo tukiingia kwa Baraka zetu kwamba sisi hatuoni kwamba Yesu hujitokeza kwa kila hitaji karibu nasi na kwamba, kama mfuasi wa Kristo sisi tumeitwa kuangalia katika vitendo.

Bwana, tusaidie kuwa makini, kukuona kwa mahitaji ya majirani wetu, kutoka kwenye ukanda wafaraja zetu na kuongozwa kufanya kitu kwake, kwa sababu ya njia hii tunaheshimu jina lako, Amina.


## MEJA VALESKA JARA

TERITORI YA AMERIKA KUSINI MAGHARIBI

Meja Valeska Jara kwa sasa anahudumu kama afisa mwenye amri kikao cha Central Santiago, Chile, na kama Katibu wa Misheni katika Sehemu ya kati ya Chile.




# TAFUTA KILE KILICHO KIZURI

AMOSI 5:10-15
ROSY KEANE

Amosi alikuwa mkulima wa kondoo aliyeishi wakati mwingine karibu 760 KK (Kabla ya Kristo), na alikulia inje ya kazi ya 'kila siku' kwa kutabiri gadhabu kubwa ya mungu kwa udhalimu unaofanyika katika taifa jirani. Sio tu kwamba Mataifa walikuwa wakiwakandamiza majirani zao kupitia vita na unyonyaji, lakini watu wa Mungu wenyewe katika Yuda na Israeli walijiunga ndani!

Katika Amosi 3:2, "Mungu analalamika, Wewe tu nimekuchagua juu ya familia zote za dunia, kwa hiyo nitakuadhibu wewe kwa dhambi zako zote. Mungu amepangilia jinsi watu wamekuwa wakiumiza wenzao na kutumia walio chini kwa faida yao "

## HAZINA YENYE NGUVU JUU YA WAHITAJI.

"Unawatoza kodi ya nafaka kwa maskini na unaweka kodi kwa nafaka zao" Kwa hivyo, ingawa wewe umejenga makao ya jiwe wewe hutaishi ndani, Ingawa umepanda shamba la mizabibu, hautakunywa mvinyo wao (Amosi 5;11)

Wakati wa kutengeneza divai, watu wangesimama juu ya zabibu hadi tunda lilipopondwa na wangeweza kufaidika kutoka kioevu ndani, Kwa njia hiyo hiyo, matajiri walikuwa wakikaa juu ya maskini hadi walipokufa, ili kupata faida kwa Wenyewe. Mahakama zilikuwa mbovu na uzito wa hakikisho ulikuwa hauna uaminifu – hakuna mtu aliyepata fursa ya kesi yao kusikika. Wenye nguvu walikuwa wanashindwa kupea haki, wakiwanyamazisha waaminifu, wakiumiza wasio na matumaini na kuwadharau walio na unyonge.

Lakini dhambi haikuishia hapo, Amosi anarekodi Waisraeli akiwaambia manabii kukomesha unabii (Amosi 2:12). Kujenga madhabahu ya juu ya ibada na kupuuza wito wa Mungu wa kuishi katika Upendo. Walikuwa wanajaribu kumnyamazisha na kumuasi juu ya Mungu, pia.

Labda wao walifikiri Mungu hatajua.?


## DINI YA NJE HUKU IKIWAUMIZA WENGINE.

Na osha vyombo katika nyumba yangu, na kitu kimoja ambacho ni kigumu sana kutoka ni siagi ya karanga. Ikiwa siko makini kijiko cha karanga siagi bado juu yake kinaweza ishia katika kabati bila kung'ara! Upande mmoja huonekana safi lakini upande mwingine sio. Itafanya kila kitu kingine kiwe kichafu na inaweza kukufanya wewe kuwa mgonjwa ikiwa wewe utapuuza. Yesu anazungumzia kuhusu kiroho na kijiko kichafu katika mathayo 23:2 anasema 'ole wenu waandishi na mafarisayo wanafiki kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na sahani na ndani yake vimeejaa unyanganyi na kutokuwa na kiasi'.

Katika kitabu cha Amosi Waisraeli wako katika hali hiyo, wao wanaendelea kuonyesha ishara ya inje ya ibaada, lakini walikuwa hawapei kipaumbele na makini kwa Mungu, Wao wanaweza kuonekana kwa kutii, lakini wanafurahia katika udhalimu na maovu, wao walikuwa wanakua wagonjwa na udhalimu.

Mungu anasema "Songa mbali na kelele ya wimbo wako, sitasikiliza kwa mziki wa vinubi vyako, lakini acha haki izunguke/*itelemke* kama mto, haki kama mkondo usio shindwa (Amosi 5:23-24).

**'IKIWA SISI TUNATAKA KUISHI, NA KUTAFUTA UZURI, TUNAHITAJI KUISHI KWA KUMTAFUTA MUNGU.'**



**KUJADILI:**

- Ni nini baadhi ya wasiwasi wako katika jamii yako ambapo wenye nguvu hukosa juu ya wahitaji? Ni kitu gani unachoweza kufanya ili kuleta mabadiliko?
- Kuna nyakati unajaribiwa kutenda dini ya nje, lakini ndani haupeani umuhimu makini' kwa Mungu?
- Je, unatambua zaidi kuwa hasira ya Mungu au huzuni ya Mungu?
- Unaweza kufanya nini ili 'kutafuta mema', na ni wapi nuru ya Mungu bado inahitajika kung'ara maishani mwako?

Hata hivyo, katikati ya hasira kuu ya Mungu, pia tunashuhudia huzuni kubwa ya Mungu kwa wingi, dhambi nyingi za watu. Katika Amosi 4:11, Maombolezo ya Mungu ni kwamba watu bado hawajamrudia Mungu.

**TAFUTA KILICHO KIZURI.**

Lengo la Mungu halikuwa tu kuwaadhibu mataifa kwa kufanya makosa; Mungu anataka watu waungane na utimilifu wa familia ya Mungu. Mungu hutoa njia ya kwa wale ambao wanataka kugeuka kutoka kwa njia zao za uovu. Jinsi tunahitaji kutafuta 'uzuri'.

Tafuteni mema wala si mabaya ili mpate kuishi, hivyo Bwana Mungu wa majeshi, atakuwa pamoja nanyi, kama msemavyo (Amosi 5:14).

Na ni nini 'kizuri'? Mema ni haki ambayo ina mtazamo wa uaminifu wa mwanadamu akilini.

'Haki' inatokana na neno la msingi ambalo linafanana na ukweli'. Tunapotafuta haki, kutoka kwa wengine au sisi wenyewe, tunataka sehemu zote za ukweli kuja kwenye nuru. Hatutaki chochote kilichofichwa. Tunajua mtu yeyote anaweza kusamehewa, hata na wadhalimu ikiwa watageuka na kumtafuta Mungu. 1 Yohana 1:7 inasema, "tukienenda nuruni kama yeye alivyo katika nuru twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu mwana wake yatusafisha dhambi yote."

Ikiwa tunataka kuishi kwa kutafuta mema, tunahitaji kuishi kwa kumtafuta Mungu. Tunahitaji kuruhusu nuru ya Mungu kung'ara ndani ya maisha yetu wenyewe ili tuweze kuangaza njia kwa wengine tunapotetea haki. Basi haitakuwa tendo la nje; Mungu kwa kweli atakuwa pamoja nasi tunaposema Mungu yuko.

Mshairi Maya Angelou anasema, 'Ninaamini hili: zuri kufanyika mahali popote ni zuri kufanyika kila mahali. Kwa ajili ya mabadiliko, anza kwa kuzungumza na watu badala ya kutembea nao kama wao ni mawe ambayo hayajalishi. Kwa muda mrefu kama wewe ungali unapumua, hatuja chelewa kufanya baadhi ya mambo mazuri.



Neno lako linasema 'usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema.' (Warumi 12:21), hivyo nisaidie kutafuta mema na kumtafuta Mungu katika mambo yote, kwa uwezo wa Roho Wako Mtakatifu. Amina.

## ROSY KEANE

### TERITORI YA NEW ZEALAND, FIJI, TONGA NA SAMOA



Rosy ni nabii, mshairi na mtakatifu kimapenzi. Anatafuta uzuri mkali wa Mungu katika viumbe vyote na watu, na anaelezea hili kwa njia ya neno lililonenwa, ambalo amefanya Kimataifa. Yeye ni mtaalamu wa rasilimali na jumuiya ya mtandaoni kwa ajili ya Jeshi La Wokovu New Zealand, Fiji, Tonga na Samoa Idara ya Wanawake, na imani yake thabiti ni kwamba Mungu anawaita wanawake katika Mwili wa Kristo kusimama, kutangaza ujumbe wa Ufufuo na kuongoza. Rosy ni askari aliyejitolea wa Kikao cha Upper Hutt na ana Wanawake wengi wakina wokovu katika ukoo wake wa whakapapa(*linage*). Rosy na mumewe Scott wameoana kwa miaka saba.

# UBUNIFU WA HAKI YA JAMII

MATHAYO 7:7-12
KAPTENI PERITA WABOMBA

**‘Ombeni, Nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa, kwa maana kila aombaye hupokea naye atafutaye hupata, naye abishaye atafunguliwa, nani kwenu, akiomba samaki atampewa nyoka, Basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema je si zaidi sana baba yenu alie mbinguni atawapa wao wamwombao? Basi yoyote myatakayo mtendewe na watu nanyi watendeeni vivyo hivyo, maana hiyo ndiyo torati na mabii’ (Mathayo 7: 7-12).**


Haki ya kijamii inapatikana wakati kuna usambazaji sawa wa mali, nafasi na mapendekezo katika jamii. Mapambano ya haki za kijamii husababisha watu kuingia katika dhambi, ufisadi na uovu, na kusababisha wengine hawapokei kile kilicho sawa kwao. Mapambano ya haki za kijamii yahimiza mifumo ya kijamii kutenda haki kwa kila mwanajamii ili watu wote waweze kuishi na kuishi vizuri. Haki kati ya watu wa Mungu ni tamaa yake: 'Hivyo katika kila kitu, fanyeni kwa wengine kile ungefanyiwa, kwani hii inajumlishwa sheria na Manabii (Mathayo 7:12).

Katika Zaburi 9, Biblia inaonyesha haja ya wale wanaodhulumiwa kumgeukia Mungu katika maombi, na anahukumu Kwa kupendelea wanaodhulumiwa: 'Bwana hutawala milele; ameanzisha kiti chake cha enzi kwa ajili ya hukumu. Anatawala ulimwengu katika haki na kuwahukumu watu kwa usawa' (Zaburi 9: 7-8).

**'KATIKA KILA KITU, FANYA KWA WENGINE KAMA VILE UNGELIPENDA NAO WANAKUFANYIENI.’**

Katika Isaya 1: 2-9, Bwana anahukumu Israeli, na agano kusambaza masharti ya kumbukumbu. Katika hatua hii, watu wa Israeli walikuwa watenda dhambi ni mahali palikuwa na ufisadi mkubwa na uovu. Mungu daima hutenda kwa haki kwa sababu yeye ni mwenye haki kwa asili. Katika haki hii ya kiungu, Mungu aliwaita Israeli kuwa watu wake. Waliwekwa katika agano na walitaka kuwa katika uhusiano mzuri na yeye kwa njia ya imani. Kwa hiyo, walitarajiwa kuishi katika uhusiano sahihi na kila mmoja na pia na watu kutoka mataifa mengine. Wito huu haukumsamehe mwanachama yeyote wa jamii, kwa kuwa hata mfalme aliitwa katika uhusiano sahihi Kwa Mwenyezi Mungu, ili awashawishi na awaongoze watu wake na mataifa jirani.

Katika siku za Yesu duniani, alitumia ushawishi wake mtakatifu kufundisha katika njia za haki ya kijamii. Kupitia mafundisho yake, wafuasi wake kugundua kwamba kuishi kwa haki kunamaanisha kuishi katika uhusiano na Mungu, pamoja na kuimarisha haki katika mahusiano na Wengine. Katika kufanya hivyo, tutatii amri ya Yesu kwa 'wafanyie wengine kile ungewataka wakufanyie' (Mathayo 7:12). Hii ina maanisha kuwatendea wanadamu wenzako kwa upendo na kuwaheshimu na kukabiliana na mahitaji yao.



**KUJADILI:**

- Vipi Yesu alipigania haki ya kijamii? Je, mbinu zake zinafaa leo?
- Jinsi gani, Unajitahidi kuishi kwa haki ya kijamii kama Mkristo?
- Jadili wakati ambapo umepatikana kwa mtu mwenye mahitaji. Uliwezaje kuwaunga mkono?

Kanisa limejitolea kutangaza misheni na ujumbe wa Yesu kwa ulimwengu mzima, hasa huduma ya amani na upatanisho. Kama Jeshi, tukipigania ujumbe huu wa kiungu, lazima tufanye kazi za upendo na huruma na kutafuta haki kwa kila mtu, kwa gharama yoyote. Kama wanawake wa Kikristo, tuna jukumu muhimu na la kinabii katika kusema ukweli. Kwa kukiri ubinadamu na karama zetu zilizotolewa na Mungu, tunazidi kuimarisha injili. Wanawake wanakabiliwa na jukumu la kutetea na kuiga haki ya kijinsia katika Kanisa na katika jamii pana.

Lengo la haki ya kijamii katika Biblia linaonyeshwa kupitia watu ambao Yesu aliwachagua kumzingira. Hakujikusanya na watu walioheshimiwa kama wastahiki, lakini anachangamana na umati wa watu wa jamii. Yesu anaruhusu watoto wadogo kuja kwake (Marko 10:14), anaonyesha huruma kwa mwanamke anayesumbuliwa na uvujaji wa damu (Luka 8:47), na anageuza maadili ya ulimwengu juu chini kwa kufundisha maadili ya Ufalme wakati anatoa Mahubiri ya Mlimani. Kama wafuasi wa Kristo, tunapaswa kuendelea na kazi ya Yesu ya kuwapenda wasiopendwa

Ni wajibu wa Kanisa kutunza yeyote au chochote kinachohitaji msaada. Ni kwa Mungu kuamua kile kilicho cha haki, na tunaweza kufanya kazi kutambua kwamba kwa njia ya kumfuata. Kama wafuasi wa Kristo, na kwa hiyo, kuwawezesha waadilifu wa haki za kijamii, lazima tupigane kwa haki katika jamii. Je, utajitolea kutunza mazingira? Je, utatetea dhidi ya maovu ya kijamii kama biashara ya binadamu na utumwa wa kisasa, dhabihu ya Watoto na unyanyasaji wa majumbani? Je, utaishi maisha ambayo ni tofauti na vurugu, uhalifu na vita? Je, utawajali watu walio na hitaji? Kwa maskini? Kwa wagonjwa? Kwa mkimbizi? Kama jirani yako anaomba mkate, je, utampa jiwe, au utampa msaada alioomba?

Baba, kwa gharama yoyote, nifanye chombo maalum cha upendo wako, amani na upatanisho. Ruhusu haki kutiririka/*kutelemka* kama mto katika mataifa yote ya ulimwengu na haki yako kama mkondo wa mto usiokuwa na mwisho. Amina.

## KAPTENI PERITA WABOMBA

TERITORI YA UGANDA



Kapteni Perita Wabomba kwa sasa anahudumu kama Katibu wa Utawala kwa Vyama vya Wanawake Uganda. Anasema, 'Kazi yangu ni fursa iliyotolewa kwangu na Mungu, kupitia ushauri wa viongozi wetu wa Teritori na idara ya Vyama vya Wanawake. Ni jukumu kubwa na lenye changamoto, ila mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.'

# KUKUA KATIKA KRISTO

WAEBRANIA 6:1-12

KAPTENI SARAH ILSTERS

Nilipokuwa mjamzito na binti yangu, nilijiandikisha Kwa barua pepe ya kila wiki ili niweze kufuata ukuaji na maendeleo ya maisha mapya ambayo yalikuwa yanaundwa ndani yangu. Alipozaliwa, nilikuwa na hamu ya kuona jinsi alifikia hatua tofauti katika kile alichoelewa na kile angeweza kufanya. Wakati mwingine nilikuwa nikisubiri na kukosekana kwa uvumilivu ili kuona jambo linalofuata! Tunaona katika kifungu hiki kwamba maisha ya kiroho yanapaswa kuwakilisha maisha ya kimwili.


Waebrania 6:1-12 inaanza na neno 'kwa hiyo'. Neno hili daima linatuelekeza kwenye nakala iliyotangulia na kuangalia kwa Waebrania 5:11-14 tunaona kwamba mwandishi wa barua hiyo amekatishwa tamaa na wapokeaji wa barua hiyo. Wao ni wa 'polepole kujifunza', kwa sasa 'wanapaswa kuwa waalimu', wamekwama kwenye maziwa – ukweli wa msingi wa Neno la Mungu, wakati lazima wapate kukomaa kwa chakula kigumu. Kujipa mafunzo kwa kutofautisha kati ya mazuri na mabaya. Hili ni suala la utambuzi/unabii na linahusisha dhamira zetu, hisia, akili na miili yetu. Tunaweza kutambua kitu kinachotujaribu kabla ya kututega? Je, tunaweza kutofautisha kati ya matumizi sahihi ya Maandiko na moja ya makosa? Je, kwa kweli tunaona hali zinaendelea kutuzunguka na kuelewa jinsi Mungu anavyotaka tupiganie haki? Lengo la maisha yetu na Mungu sio tu kuokolewa. Tunapaswa kukua, kukomaa, kufundisha, kwenda zaidi katika Neno la Mungu kwa kuchukua hatua zinazoathiri ulimwengu unaotuzunguka.

Watu waliopokea barua hii walikuwa wale walioagizwa katika imani ya Kiyahudi, walikuwa wakilenga pamoja jinsi imani mpya katika Kristo kama Masihi alivyokwenda pamoja na kuelewa kwa mazoea yao ya Kiyahudi. Hata hivyo, walikuwa wamekwama kubishana juu ya misingi, badala ya kutegemea kikamilifu juu ya Kristo na kuweka nguvu zao zote katika kuishi kwa ajili yake na kukua kama yeye. Mafundisho ya msingi ya imani yetu ni muhimu: umuhimu wa imani, si kujaribu kuokolewa na kile tunachofanya, kuelewa umuhimu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, ufufuo na uzima wa milele (Waebrania 6:1-2). Lakini ukomavu unatuhitaji kukua zaidi, kuwa na ujuzi kamili wa Maandiko, miereka na mtazamo mpana wa Mungu ni nani na kile anachohitaji kutoka kwetu.

**‘TUTAKUWA TUKIKUA KATIKA KI TABIA KAMA KRISTO KUFANYA KAZI KWA HAKI, NA SISI TUTAHUSIKA KATIKA KUONA UFALME UNAKUA.’**

Nia ya awali ya mistari 4-6 ingekuwa kuonya Wakristo wa Kiebrania ambao, wakiwa wamemkubali Kristo mara moja, walichagua kurudi Uyahudi na hivyo kufanya uasi. Kuna maoni tofauti kuhusu mistari hii leo - ni watu hawa ambao wakati mmoja walikuwa Wakristo na kugeuka, au ni watu wagani ambao kamwe hawakuwa Wakristo? Baadhi ya Wakristo walisoma mistari hii na hasa maneno 'haiwezekani... kuwa kurudi kwenye toba' na wasiwasi kuna kitu wanaweza kufanya ambacho kinamaanisha hakuna njia ya kurudi kwa Kristo. Hata hivyo, ujumbe mkuu hapa ni kwamba hawa ni watu ambao wanamkataa Kabisa Kristo – haiwezekani kumkataa Kristo na kuokolewa. Hakuna njia nyingine ya kuokolewa mbali na imani katika Msalaba. Kuna ugumu wa moyo unaoifanya haiwezekani kwa mtu kutubu.

Kisha kuna picha ya bustani mbili - zote zin uzoefu wa mvua inayonyesha mara nyingi (Mathayo 5:45), bustani moja hutoa mazao 'muhimu kwa yeye anayelima', nyingine



**KUJADILI:**

- Uko wapi sasa hivi katika uhusiano wako na Mungu? Je, umekwama na mambo muhimu? Je, umemgeukia Mwenyezi Mungu? Je, unafundisha kila siku katika kutofautisha mema na maovu?
- Ni matunda gani mazuri unaona kukua katika maisha yako?
- Watu walio karibu nawe ambao Mungu anakuita ukusaidie? Wapi unaweza kufanya kazi kwa haki sasa uko wapi?

Haina maana 'miiba na michongoma'. Picha hii inarudia mafundisho ya Yesu kuhusu miti na matunda. Anasema mti mzuri hauwezi kuzaa matunda mabaya, na mti mbaya hauwezi kuzaa matunda mazuri. Hivyo kwa matunda yao mtawatambua. Yetu nayo ni bustani. Kama tunakomaa kwa imani 'mazao' yetu au matendo yetu, mambo tunayoyafanya maishani, ni muhimu kwa wale walio karibu nasi. Tutakua katika tabia kama ya Kristo, tukifanya kazi kwa ajili ya haki na tutahusika katika kuona ufalme wa Mungu unakua. Tukichagua kutokua, tuko katika hatari ya kuzalisha miiba na michongoma ambayo haitumiki kwa mtu yeyote. Haya ni maneno magumu ya kusoma - lakini ni manufaa kwamba tunaweza kuona kwa uhakika matokeo ya kusimama tu na si kukua, au kugeuka mbali na Kristo.

Katika Maandiko yote Mungu ana ndoto - kuwa na watu wanaompenda, wanatafuta kumwelewa na wanataka kufanya kazi pamoja naye ili kuona mapenzi yake yakifanywa duniani kama ilivyo mbinguni. Mwandishi kwa Waebrania alikuwa na ujasiri kwamba wasomaji wake walikuwa sehemu ya timu ya ndoto ya Mungu - kwamba wangeendelea kutoka kwa ujuzi wa mafundisho ya msingi kwa maarifa ya kweli ya kina. Anawapongeza katika mstari wa 10 kwa kazi na upendo waliouonyesha kwa watu wa Mungu. Na wanakumbushwa kwamba Mwenyezi Mungu si mwenye kudhulumu, lakini anakumbuka mema yote, tunayoyafanya tunapomfanyia kazi na kuwapenda watu kwa jina lake. Waumini hawa walikuwa wanawasaidia waumini wengine – ndugu na dada zao katika Kristo, labda wakati mwingine kujiweka katika hali ngumu. Kazi pamoja na kuwapenda ndugu na dada zetu duniani kote ni muhimu tu leo – kuwasaidia wale ambao wanateseka na katika hali ngumu na wakati mwingine hatari. Sisi sote ni sehemu ya timu ya ndoto ya Mungu na kwa njia hiyo ni sehemu ya kila mmoja. Mafungu haya yanaishia na wito wa uvumilivu, kutokuwa wavivu. Jinsi tunaweza kuendelea kukua na kukua katika uhusiano wetu na Mungu na upendo wetu kwa wale walio karibu nasi? Lazima tuwe daima tuangalie Neno la Mungu kutuhamasisha na kutuongoza na lazima tuchukue hatua, tusiwe wa kupendeza, bali tutende kwa haki katika hali ambayo Mungu ameweka kila mmoja wetu.



Yesu, maisha yangu yaweze kuakisi(reflect) maadili yako na kamwe siwezi kukosa uvumilivu wa kuendelea kuwa mfuasi mkomavu.


## KAPTENI SARAH ILSTERS

TERITORI YA USWIDI NA LATVIA


Kapteni Sarah Ilsters ni Kiongozi Msaidizi wa Mkoa mwenye jukumu la mafunzo katika Latvia. Pamoja na agizo lake la sasa, amefanya kazi katika idara za watoto na vijana hufanya kazi na kuongoza vikao. Sara ameolewa na Aivis na wana watoto wawili. Kwa wakati wake wa ziada anapenda kusoma, kuchunguza mazingira yake na kuwa na mazungumzo ya maana.



# HUZUNI YA KIMUNGU INAELEKEZA KWA VITENDO

2 WAKORINTHO 7

KAPTENI SUMMRA NEMAT

Ni mara ngapi kwa siku unasikia mtu akisema 'samahani'? Mara nyingi watu hutumia neno hili kuepuka madhara ya matendo yao, au kwa sababu wanajuta kukamatwa. Rafiki yangu asema 'samahani' tu, ili kumaliza mazungumzo na kuepuka hoja.

Paulo, katika barua yake kwa Wakorintho, huleta tofauti wazi sana kati ya huzuni ya kimungu na kidunia. Anasema huzuni ya kimungu huleta toba ambayo inaelekeza kwa wokovu na haiachi majuto, lakini huzuni ya kidunia huleta kifo. Huzuni ya kimungu hufanya kazi kwa njia hii: huzuni kwanza, kisha toba na hatimaye, maisha yaliyobadilika.

Kwa nini Paulo alitaja tofauti kati ya huzuni ya kimungu na huzuni ya kidunia kwa Wakorintho? Kulikuwa na mambo mengi yanayoendelea huko Korintho ambayo yalimfanya Paulo kuwakabili. Kanisa lilikuwa dhaifu, linapambana na mgawanyiko na uchanga wa kiroho. Wengine walimpinga Paulo na kuhoji uthibitisho wake.

Matatizo mengi na changamoto zinazolikabili kanisa la Korintho ni sawa na zinazotukabili leo. Sisi huhukumu kila mmoja ambaye huweka mgawanyiko katika Kanisa. Kazi yetu inapaswa kuwa umoja wa Kanisa, si kuwa mgawanyiko na kuua Kanisa na sio kuunda vikwazo. Mtazamo wa hukumu unatuondoa kwenye wajibu wetu ambao ni kuwalete watu kwa Mungu.


Paulo alisikitishwa na kuandika barua ngumu kama hiyo kwa Wakorintho kuhusu dhambi. Katika safari ya maisha yetu, sisi pia katika uzoefu wa ugumu huu, na inaonekana vigumu kusema ukweli wakati ukweli haupendezi. Hatujisikii vyema juu ya kufanya hivyo, lakini kama waumini tunapaswa kufanya hivyo, kwa sababu wakati mwingine maneno magumu yanahitaji kusemwa na kama wafuasi wa Yesu lazima tufanye kile ambacho Mungu ametuita kufanya: kupenda nafsi ya mtu.

Hii inaniongoza kutafakari juu ya maswali haya: Kama waumini, tuna mtazamo wa aina gani? Je, tuna mtazamo wa hukumu dhidi ya wengine?

Paulo alipopokea habari njema kutoka kwa Tito kwamba wengi huko Korintho walikuwa wametubu na kulikuwa na wachache tu na kundi la kindugu ambalo lilikuwa likiendelea kusababisha matatizo, Paulo aliwahimiza waumini wa Korintho kuhusu kanisa na nidhamu ambayo ilisaidia kuleta wengi katika toba.

Toba huja tu wakati tunaweza kuona kwamba dhambi ni chungu kwa Mungu. Tunapogundua kwamba dhambi ni kikwazo kwa utakatifu, tunapata huzuni wa kiungu. Huzuni ya kimungu ni motisha ya kujiona wenyewe jinsi Mungu anavyotuona na kutusaidia kutubu na kujipanga wenyewe kuwa zaidi kama Kristo. Huzuni hii inatulazimisha kutubu na kutafuta utakatifu wa Mungu.
Zaburi 51:4 inatuhakikishia: 'Ninyi tu, mmetenda dhambi, na kutenda yaliyo mabaya machoni pako.' Daudi alikiri kwamba alikuwa ametenda dhambi na alikuwa amefanya kile kilichokuwa kiovu machoni pa Mungu. Huzuni ya kimungu inaelekeza kwa toba ya kweli ambayo haijalishi kuhusu matokeo lakini unataka tu mambo yafanywe sawa na yanahusika zaidi na Mungu kuliko nafsi yake.
Paulo alikuwa anawaalika Wakorintho kujitakasa wenyewe kutokana na kila kitu kinachochafua mwili na roho, kukamilisha utakatifu kutokana na heshima kwa Mungu, ambayo ni hatua mbili: alikuwa anawaomba wajiondolee dhambi na kumgeukia Mungu, kufanya kazi na kuelekea utakatifu, kukomaa katika imani. Paulo alikuwa anawaomba waishi katika dunia hii lakini si kutenda kama dunia hii. Imeandikwa katika Warumi 12:2, 'Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu,'. kutokana na ajenda hii twahitaji kutakaswa kisha tutaona utofauti.

**'MATATIZO NA CHANGAMOTO NYINGI ZINAZOLIKABILI KANISA LA KORINTHO NI SAWA NA YANAYOTUKABILI LEO.'**



**KUJADILI:**

- Fikiria juu ya mtu ambaye anafanya vibaya. Unataka kusema nini kwa mtu huyo? Uliza Roho Mtakatifu akusaidie kusema ukweli kwa mtu huyo.
- Ikiwa 'huzuni ya kiungu' inaelekeza kwa toba, tunawezaje kuzalisha hii 'huzuni ya kimungu' kwetu sisi wenyewe na wengine?
- Fikiria juu ya udhalimu unaotokea karibu nawe. Unaweza kutumia kanuni ambazo Paulo anaelezea katika 2 Wakorintho 7:11?

Ili kuishi maisha matakatifu, tunahitaji kufungua safu nyingini na kujichambua wenyewe. Sisi ni wema sana katika kujidanganya wenyewe, lakini tunahitaji kuwa wakweli. 2 Wakorintho 7:11 inaelezea vizuri sana,'Maana, angalieni, kuhuzunishwa kuko huko kwa jinsi ya Mungu kulitenda bidii kama nini ndani yenu; naam, na kujitetea, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam na shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi! Kwa kila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hili.

Huzuni ya kimungu hutoa bidii na hamu ya kufanya kitu kuhusu makosa yaliyofanywa, kama sehemu ya toba ya kweli. Pia inatoa hamu ya kujiondoa wenyewe na hamu kubwa ya kufuta jina letu, au kujikwamua kwa hatia na aibu, na kujithibitisha wenyewe kuwa waaminifu tena. Zakayo ni mfano katika Luka 19:8, kutoa tena mara mbili kiasi alichokuwa amechukua.

Hamu ya kujithibitisha wenyewe kama waaminifu na wenye haki tena inaonyesha hofu. Baadhi ya tafsiri hutumia neno 'kengele'. Tena, msisitizo ni juu ya hatua. Kuna kutamani na ari ambayo huchochewa mara moja ndani ya mtu. Haki ya kusahihisha makosa, na kujirejesha wenyewe kama waaminifu kweli kweli. Wazo linaendelea katika sentensi inayofuata: 'Katika kila hatua umejidhihirisha kuwa huna hatia katika jambo hili.'

Tuko tayari kwenda hatua zaidi kufanya vizuri?

Baada ya kujichambua wenyewe kupitia lensi ya Maandiko tunaweza kwenda zaidi katika uhusiano wetu na Bwana, kisha tunaweza kuona ni dhuluma gani kama tulikuwa vipofu kwazo.

Wakorintho walishughulikia dhiki yao na kusahihisha dhambi vizuri. Walikubali kwamba walikuwa wamekosea na walijibu haraka na jibu la Mungu la huzuni, hamu, bidii na hamu ya kile kilicho sahihi.

Ninakumbushwa kwamba upendo wa Mungu ni kwa sisi sote (Yohana 3:16), lakini sote tumetenda dhambi (Warumi 3:23) na kutakuwa na matokeo kama hatutatubu!

Kama wafuasi wa Kristo tunaitwa kuonyesha tabia yake na 'kufanya haki'. Tumeitwa kuchukua hatua. Tunaitwa kukabiliana na uovu na kufanya mema na kubadilisha mabaya kuwa mema.

Mpendwa Bwana, upendo wako na imani ya Roho Mtakatifu utuwezesha kutenda haki kuhusu mtazamo wetu wenyewe, na tunaweza daima kutafuta haki kwa wengine. Amina


**KAPTENI SUMMRA NEMAT**

TERITORI YA PAKISTANI

Kapteni Nemat ni Katibu Msaidizi chini ya Katibu wa Ukanda wa Asia kusini katika Makao Makuu ya Kimataifa, London.




# MOYO WA HAKI

AMOSI 5:24

LUTENI VERÓNICA CENTENO

Tunaposikia kisahazi(phrase), 'Yeye ni mtu wa Mungu', tunafikiria wainjilisti maarufu, wachungaji, wamishionari, fikiria juu ya wale watu wa Kikristo wanaohubiri na kufundisha Neno la Mungu kwa sababu ya wito wao. Amosi alikuwa mtu wa Mungu ambaye alijitolea kumtumikia Bwana na maisha yake alionyesha wito wake. Amosi aliona maisha kama kitu cha kudhibitiwa na Mungu wa haki. Katika karne zote, ujumbe wa Amosi umeathiri watu wa Mungu. Wakati huu pia mataifa yanahitaji kusikia ujumbe wake pia.

Kwa hiyo, kama Wakristo, tunaelewa nini kwa 'haki ya kijamii'? Kiini cha haki ya kijamii ni usawa, usambazaji wa yote yanayochukuliwa kama manufaa ya wote ndani ya jamii, kwa kuzingatia usawa, fursa sawa na kuheshimu haki za binadamu.

Mungu aliongea kupitia Amosi kwa kishazi(phrase) kinachojulikana sana, kwamba mkusanyiko huu wa masomo ya Biblia unaitwa kwayo, 'Lakini hebu Haki itelemke kama mto, haki kama mkondo usioshindwa kamwe! (Amosi 5:24). Kubiringishwa huku kwa haki kama mto na haki kama mkondo hutufanya tufikirie juu ya haja ya kuwa na sheria za haki na kisha kuzitumia Vizuri.

**'WAKATI MWINGINE TUNAHITAJI SANA UJASIRI KWA KUFUATA ZAIDI KUPITIA KWA KILE MUNGU ANATUULIZA.'**

Na mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kuyaona hayo wayatendayo. Ni kuhusu kanuni sahihi za maadili za haki na tabia njema kwa watu wengine, aina ya tabia ambayo inawapa wengine fursa ya kupata uzoefu mzuri na kutokana na jinsi tunavyotenda. Nabii anasihi kwamba mioyo na maisha ya watu yawe yanayoongozwa na maadili na njia ya kuishi iliyowekwa katika Neno, badala ya kufuata njia ya ulimwengu. Ili haki ya kubingirisha kama mto, na haki kama kijito, lazima tupate ujasiri wa kufanya kile kilicho sahihi.


Katika wakati wake, Amosi alitazama moyo wake kwa moyo wa Mungu na alilaani udhalimu kama alivyoona: alizungumzia kuhusu mfumo wa mahakama ya kifisadi ambapo majaji walikubali kutoa rushwa na alitangaza asiye an hatia kuwa na hatia (Amosi 2: 6-12).

Alizungumzia kuhusu kundi la matajiri ambalo liliwaangalia maskini. Lilikuwa kundi la kijamii ambalo lilifurahia kuona taabu ya maskini, na waliozuia njia ya wanyenyekevu na wasiojiweza (Amosi 2:6-7; 3:10).

Alizungumzia kuhusu ngano na mkate. Walikuwa watu ambao hawakujali njaa na mahitaji ya watu, sio hata kuhusu mambo ya msingi zaidi kwa wanadamu kuishi juu yake (Amosi 8: 4-6).

Je, usifikiri mambo mbalimbali ambayo Amosi aliyazungumzia bado ni ukweli katika siku zetu? Nabii anatualika kutafuta kutenda mema na sio uovu, kuchukia uovu na kuwa na upendo kwa wote (Amosi 5:14-15).

Katika agizo langu la sasa, ninawahudumia wanawake walio katika mazingira magumu ambao wametafuta makazi na faraja katika vituo vyetu. Kila wakati mimi huzungumza na wanawake wanaoishi katika nyumba zetu, ninaona udhalimu.



**KUJADILI:**

- Je, haki inayoongozwa na binadamu inaweza kulinganishwa na haki inayoongozwa na Mungu?
- Je, ni kushindwa gani tunaona leo katika haki ya kijamii ambayo haizingatii mapenzi ya Mungu?
- Kanisa lina jukumu gani katika kupigania haki ya kijamii?

Ninawasikia wakisema: 'Sikuweza kupata kazi kwa sababu ninaishi mtaani' au 'Sijamaliza masomo yangu – Sina viwango, sina sifa. Kawaida kama watafaulu kupata kazi, wanajikuta katika mtego wa leba unyonyaji, kupata malipo kidogo sana, lakini kufanya kazi masaa marefu sana.

Katika nafasi ya kwanza, si sahihi kwamba walipaswa kuwacha nyumba zao, watoto wao na, wakati mwingine, hata nchi zao wenyewe. Lakini hii ni hali ya ulimwengu wetu. Kutokana na unyanyasaji wa majumbani na vitisho, wanawake wengi huishi katika hali ya udhalimu mkubwa. Wanawake katika timu yangu wamelazimika kuchukua kimbilio huku wakiendea matibabu ambayo yatawasaidia kutokana na hofu na wasiwasi, na wanaweza kurekebishwa wawe huru.

Amosi aliongea kwa uaminifu sana kuhusu dhambi. Alipambana na viongozi wa kidini wa uongo wa wakati wake na hakutishwa na makuhani au mfalme. Kwa ujasiri aliendelea kusema ujumbe wake kwa sauti kubwa na wazi. Je, Mungu anatarajia nini kutoka kwetu? Mungu anatarajia uaminifu, huruma kwa wengine, haki na unyenyekevu. Mengi ya mambo yaliyotokea wakati wa Amosi ni dhahiri katika jamii ya leo. Katika Amosi tunajifunza kwamba wakati mwingine tunahitaji ujasiri mkubwa wa kufuatana na yale Mungu anayotuuliza.

Tunafanye aje haki kama Kristo alivyofanya na kama wafuasi wake katika ulimwengu huu? Mungu aliwaumba watu wote. Kwa hiyo, kusahau wale ambao ni maskini, au waathirika wa ukatili wa kijinsia, au waathirika wa biashara ya binadamu, inamaanisha kwamba tunasahau wale ambao Mungu anawapenda na ambao Kristo alikuja kuwaokoa. Lazima tufanye zaidi ya kuhisi maumivu na utulivu kwa maskini na wanaoonewa. Tunahitaji kutenda kwa huruma, kuacha udhalimu na kuwasaidia wale walio na mahitaji.


Ewe Mola wangu Mlezi! Kuteseka na kutusaidia kuunda ulimwengu ambao zaidi ya mahitaji yetu wenyewe na majeraha, tunaweza kufanya mazoezi ya haki, huruma, upendo na kuwasaidia wale walio na mahitaji.

**LUTENI VERÓNICA CENTENO**

TERITORI YA MAREKANI MASHARIKI.

Luteni Verónica Centeno anahudumu sasa hivi kama Afisa Msimamizi wa makao ya nyumbani ya Amparo Y Betania. Hapa ni mahali ambapo wanawake wanaoishi mitaani hutunzwa katika hali ya jamii zisizojiweza.





THE SALVATION ARMY